tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



KESI DADA BILIONEA MSUYA
**Shahidi** aeleza binti alivyomtambua mtuhumiwa mauaji gwaride la polisi
UKURASA 19


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Ni wakati wa kutafakari vijana watakavyotumika kunufaisha taifa
ELIMU
NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA
Mabinti wanaorejea darasani baada ya uzazi wana haya...
UKURASA 11

Jumanne Agosti 22, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581410
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Samia: Nimeamua kunyamaza, sitajibu

• **Atoa** angalizo mambo matatu; Askofu Shoo atoa msimamo wa KKKT...*Uk.2*


Rais Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na maaskofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), baada ya kuzungumza nao kwenye maadhimisho ya miaka 60 ya kanisa hilo jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**

## Daktari bingwa wa moyo aliyebuni JKCI afariki dunia

UKURASA 5



Mwonekano wa Soko la Bwawani katika Mtaa wa Bwawani, Manispaa ya Kinondoni lililojengwa kwa Sh. bilioni moja ambalo limetelekezwa kwa madai ya kukosa wateja. **PICHA: JENIFER GILLA**

RIPOTI MAALUM

## Mradi wa soko ulivyogeuka 'nyonya damu' kwa manispaa

UKURASA 4

MICHEZO GAMONDI ASHANGAA KUTOSHINDA 10 UK.24 KATUNI UK.6

# Samia: Nimeamua kukaa kimya, sitajibu

Na Waandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema hakuna mwenye misuli na ubavu wa kuligawa Taifa, kuuza Taifa na kuharibu amani na usalama uliojengwa kwenye Taifa.

Vilevile, amesema aliamua kunyamaza na ataendelea kunyamaza katika suala la uwekezaji katika bandari unaotaka kufanywa na Kampuni ya Kimataifa ya DP World.

Wakati Rais Samia akitoa kauli hiyo, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, amemweleza Rais kuwa wanaunga mkono uwekezaji na wanatambua nia yake njema katika suala hilo.

Ni kauli zilizotolewa jana na viongozi hao wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya KKKT, Rais Samia akiwaomba viongozi wa madhehebu yote ya dini nchini kudumisha dua na sala kwa ajili ya nchi.

"Niliamua kunyamaza kimya na ninaendelea kunyamaza kimya, ninachotaka kuwahakikishia hakuna mwenye misuli na ubavu wa kuligawa Taifa hili, hakuna mwenye ubavu wa kuuza Taifa hili, kuharibu amani na usalama tuliyojenga kwenye Taifa hili, itoshe kuwa huu ni ujumbe wangu kwenu," alisema.

Rais Samia alitumia fursa hiyo kuwashukuru viongozi wa dini hususani Askofu Dk. Shoo na Askofu wa KKKT Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza kwa ushauri wao wa kuanzisha Jumuiya ya Maridhiano Tanzania ambayo imekuwa na tija kwa Taifa.

Kuhusu mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula, Rais aliagiza viongozi wa dini kutumia majukwaa yao kuhimiza utunzaji mazingira na kuweka mipango yao, ili kutunza mazingira na kujihakikishia usalama wa chakula.

Kukabiliana na usalama wa chakula nchini, alisema Rais Samia serikali imeanzisha mradi wa Bulding a Better Tomorrow (BBT) unaounganisha vijana katika sekta ya kilimo. Unajikita katika kilimo cha umwagiliaji, ufugaji na uvuvi, ili kupata chakula cha kutosha ndani na nje ya nchi.

**MAADILI**

Rais Samia pia aliwaomba viongozi wa dini kwa kushirikiana na serikali kuwajengea maadili mema watoto na vijana kwa kuzingatia mila na desturi njema za Watanzania, ili kuendelea kuwa na Taifa lenye maadili mema.

Mkuu wa Nchi pia alisema serikali inatambua mchango wa makanisa katika utoaji huduma za jamii, hasa afya na elimu, uwezeshwaji wananchi kiuchumi na utoaji huduma shufaa na itaendelea kushirikiana nazo, ili wananchi wapate huduma stahiki.

"Kuhusu changamoto zote ulizozisema Mkuu wa Kanisa, ninakuahidi nitazifanyia kazi na zinazojitokeza na zitakazoendelea kujitokeza ili sera ya kitaifa ya ushirikiano wa sekta binafsi (PPP) iendelee kuwatumikia wananchi," Rais aliahidi.

**ASKOFU SHOO**

Awali, Mkuu wa Kanisa hilo, Askofu Dk. Shoo, alisema: "Lipo hili la DP World. Kwanza, ninaomba ieleweke wazi kwamba kanisa linaunga mkono uwekezaji, hatupingi uwekezaji na tunajua wewe kwenye nia



yako unataka wawekezaji.

"Hata hivyo, jambo hili limekuwa na maoni mbalimbali kwa wananchi na vyombo vya habari, viongozi wa dini zote, kwenye mitandao tumeona maoni mbalimbali.

"Lakini Mheshimiwa Rais unatambua sisi viongozi wa dini zote, tuliomba kuja kukuona pale mwanzoni mwa jambo hili na kwa uungwana wako na unyenyekevu ulionao, utayari wa kutusikiliza, ulitupokea na tulikuletea maoni yetu, kama taasisi na viongozi wakuu wa dini katika nchi yetu ya Tanzania.

"Madhehebu yote ya kikristo tukiwa CCT, TEC na Bakwata. Mimi ninakumbuka jinsi ulivyotupokea, ukatusikiliza, ukapokea maoni yetu na ushauri wetu wa viongozi wa dini na uliahidi kuwa maoni na ushauri utayapeleka kwa wataalamu wako na kufanyiwa kazi kwa uzito na kwa maslahi ya Taifa.

"Tuna imani na wewe Mheshimiwa Rais, tunakuamini, kanisa liko pamoja na wewe, tutaendelea kukuombea na kukuunga mkono katika kulisukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

"Tunaendelea kuunga mkono juhudi zinazoendelea katika kutengeneza fursa zitakazowezesha wananchi kujipatia maendeleo, kwa njia ya utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu na kuruhusu demokrasia ya kweli miongoni mwa wananchi na vyama vya siasa."

Kwa mujibu wa Dk. Shoo, Rais amewewka wazi msimamo wake na wameona watu wakiwa huru, na kueleza maoni yao na ni matumaini yao kwamba watendaji wote wataelewa vyema nia yake njema na nchi itaendelea kuwa yenye amani na mshikamano.

Askofu Dk. Shoo alisema anajua katika jambo hilo, imefikia hatua baadhi ya watu wenye maslahi ya kidini na kiasisa, wanataka kuwagawa Watanzania wakati suala hilo linahitaji hekima na wao kama viongozi wa dini, wataendelea kumwombea.

"Ukimya wake (Rais Samia) katika suala hilo siyo kwamba halifanyii kazi. Umoja wa Taifa la Tanzania na mshikamano ni muhimu kuliko mtu au kundi lolote. Ninawaomba viongozi wenzangu wa dini, wanasiasa kuacha kugawa watu kwa misingi ya dini, siasa na maslahi binafsi na iwapo kuna atakayejenga hoja kutaka kugawa Watanzania kwa misingi hiyo akemewe.

"Ninashukuru Mungu amekujalia hekima kama mama na kiongozi umekaa kimya na kimya chako siyo kwamba hulifanyii kazi, jambo hili linahitaji hekima kubwa.

"Ulipokea nchi katika kipindi kigumu, ukaahidi kutekeleza miradi ya kimkakati na tumeshuhudia ukiitekeleza na kuanzisha mingine mipya, sisi viongozi wa KKKT tunakuunga mkono, tunakuomba ufanye kazi kwa kujiamini na ujasiri kwani Mungu ndiye amekuweka katika nafasi hiyo na sisi tunaieshimu," alisema.

Kuhusu maadhimisho hayo, Askofu Dk. Shoo alisema wanashukuru serikali kutambua mchango wa taasisi za dini nchini. Kanisa hilo limekuwa kutoka waumini 500,000 mwaka 1963 lilipoanzishwa hadi sasa kufikia waumini zaidi ya milioni nane, huku dayosisi zikiongezeka kutoka saba hadi kufikia 27 katika mikoa na maeneo yote nchini.

Alisema mbali na huduma za kiroho kanisa hilo limekuwa mstari wa mbele kutoka huduma za kijamii.

Askofu Dk. Shoo pia aliishukuru serikali kwa kutoa fedha Sh. bilioni tano kwa ajili ya ujenzi wa jengo la matibabu ya saratani ambao kwa sasa umefikia asilimia 70 katika Hospitali ya Rufani ya KCMC inayomilikiwa na kanisa hilo.

**BAKWATA**

Katibu Mkuu Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Mwalimu Nuhu Mruma alisema BAKWATA inaipongeza KKKT kufikia miaka 60 ya kuanzishwa kwake na itaendelea kushirikiana na madhehebu ya dini nchini katika shughuli mbalimbali zikiwamo za maendeleo.

"Sisi viongozi wa dini tutaendelea kushirikiana kwa sababu jukumu letu kubwa ni kuishauri serikali na kuwaombea viongozi, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa amani na utulivu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella alisema KKKT katika mkoa huo ni wadau wakubwa wa maendeleo ambao wamekuwa wakipeleka miradi mbalimbali kwa wananchi bila kujali dini zao.

Mkurugenzi wa Idara ya Afya ya kanisa hilo, Dk. Paul Mbando, alisema KKKT inamiliki taasisi zaidi ya 300 za kijamii, zikiwamo 120 za sekta ya elimu na 172 za afya.

Akihubiri katika ibada hiyo, Askofu wa Dayosisi ya Magharibi Kati (Tabora), Dk. Isaac Kisiri, alisema licha ya KKKT kuwa na mambo mengi ya kujivunia katika safari yake ya miaka 60, wakristo wamekuwa wavivu na kuweka imani zao katika vitu vya upako, ili wafanikiwe kiuchumi badala ya kufanya kazi kwa bidii na kumtegemea Mungu.

**SIASA NA DINI**

Katika hatua nyingine, baadhi ya wadau wa siasa, sheria na haki za binadamu nchini, wamezungumzia kauli ya Rais mstaafu Jakaya Kikwete kuhusu kuchanganya siasa na dini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema jana kuwa Katiba ya nchi inasema kila raia ana haki ya kutoa maoni.

"Huwezi kutenganisha dini na siasa kwa sababu watu wenye dini ndio haohao wanasiasa na wanasiasa pia wana dini. Kwa hiyo ukisema kiongozi wa dini asiongee kuhusu siasa, sidhani kama ni sawa. Kitu kibaya ni kuwabagua watu kwa minajili ya dini," alisema.

Mwanasiasa Mkongwe, James Mbatia, alisema: "Ni vigumu kutenganisha siasa na dini, lakini hata hivyo waraka wa TEC hauzungumzii mambo ya sakaramenti, yanazungumza mkataba. Rais alitoa rai Watanzania watoe maoni, wao wamefanya hivyo. Kwahiyo, hoja ijibiwe kwa hoja, hakuna hoja ya dini hapo."

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule Kuu ya Elimu (DUCE), Dk. George Kahangwa, alisema hata manabii wa zamani walikuwa wanaelekeza viongozi katika kuweka mambo sawa.

"Dini na siasa ndio maisha yetu. Kilicho kibaya ni kutumia mtaji wa dini kujinufaisha kisiasa, lakini huwezi kusema ndani ya dini hakuna siasa, dini ilivyokuja kwetu ilichanganyikana na siasa," alisema Dk. Kahangwa.

Askofu wa Kanisa la Baptisti, Antony Mlyashimba, alisema ni vigumu kutenganisha siasa na dini kwa sababu binadamu ameumbwa kwa mwili na roho na viongozi wa dini wana kazi ya kuhakikisha wanahudumia vyote hivyo vikae sawa bila kuharibikiwa.

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema: "Wafuatiliaji wa siasa na historia ya dini wataungana na mimi kwamba ni vigumu kutenganisha uhusiano wa dini na siasa.

"Kitu kikubwa ambacho viongozi wa dini wanapaswa kuzingatia ni kwamba wanapozungumza, maneno yao yazingatie kujenga umoja wa kitaifa kwa sababu wamebeba dhamana kubwa ya nchi."

***Imeandaliwa na Cynthia Mwilolezi (ARUSHA) na Elizabeth Zaya (DAR)**

HABARI KITAIFA

# Katibu Mkuu Kiongozi ataka ufanisi taasisi za umma nchini

**Na Jenifer Gilla**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Kusiluka, amesema taasisi nyingi za serikali nchini zinatoa huduma duni kwa jamii ikiwamo ya umeme, maji na elimu, hali inayorudisha nyuma lengo la kuwahudumia wananchi.

Pia amesema ni wajibu wa taasisi hizo kuhakikisha zinatoa huduma kwa ufanisi na pale panapotokea tatizo, wananchi wapewe taarifa na marekebisho yafanyike haraka, ili kuwaondolea wananchi usumbufu unaotokana na hitilafu husika.

Ili kuondokana na tatizo hilo, Dk. Kusiluka ameelekeza Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Mipango kutekeleze maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwamo kupitiwa upya utendaji wa taasisi hizo ili hatua stahiki zichukuliwe ikiwamo kuziongezea mitaji, kuziunganisha na nyingine kuzifuta.

Dk. Moses aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati akifunga kikao kazi cha Wenyeviti wa Bodi, Watendaji na Wakuu wa Taasisi za Umma na kusisitiza utekelezaji huo ufanyike haraka na kwa umakini mkubwa ili kuepuka taasisi ambazo zinatia hasara na kufanya kazi bila tija.

Pia aliagiza taasisi hizo zizingatie sheria na miongozo ya utendaji wa kazi serikalini na kuepuka matumizi mabaya ya madaraka waliopewa ambayo huchangia kutoa huduma duni kwa jamii.

"Tuwe makini, hili ni eneo ambalo huko nyuma hatukufanya vizuri, lakini kumekuwa na haja ya kulipitia na kuona kwamba lirejewe upya. Kwa hiyo, ni imani yangu na ya Rais kwamba mtasimama katika nafasi zenu vizuri na hatutapata shida katika suala hilo," alisema.

Alisema serikali ipo katika mchakato wa kutunga sheria mpya itakayoipa Ofisi ya Msajili uwezo mkubwa wa kusimamia uwekezaji wa serikali katika mashirika ya umma pamoja na utoaji huduma unaofanywa na taasisi za serikali.

Alisema ni matarajio ya serikali kuwa mashirika yanayofanya biashara yanatengeneza faida kubwa, hivyo yakae na Msajili wapeane mikakati, ili mwakani watakapokutana tena watoe taarifa za mafanikio na namna ya kusonga mbele.

Vilevile, aliwaelekeza viongozi wa juu wa taasisi hizo kushiriki moja kwa moja katika katika ukaguzi wa hesabu za mashirika yao, wampe ushirikiano wa karibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kujibu hoja zake kwa wakati badala ya kuwaachia majukumu hayo wafanyakazi wa ngazi za chini.

Alisisitiza taasisi na mashirika hayo kusimamia maazimio hayo, kila taasisi iyachukulie kama maazimio ya msingi kwa sababu yanalenga kutatua matatizo wanayokabiliana nayo, kuwapeleka mbele na kuongeza ufanisi wa taasisi hizo.

Katika kikao hicho, Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu alisema jina la taasisi hiyo litabadilika kuwa Mamlaka ya Uwekezaji wa Umma, ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji majukumu yao.

Alisema jina hilo linalopendekezwa litakidhi matakwa ya sheria ya mamlaka na majukumu ya ofisi hiyo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Alizikumbusha taasisi hizo kuwa miongoni mwa vigezo vya kupewa uhuru wa kujiendesha ni pamoja na maslahi na malengo ya kimkakati ya nchi, uchangiaji mapato yasiyo ya kikodi katika mfuko mkuu wa serikali na uwezo wa kujiendesha kwa mapato ya ndani ya taasisi kutegemea serikali.

# Mwabukusi, Mdude waibuka na hatua mpya zuio kutoka Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKILI Boniface Mwabukusi na mwanaharakati Mpaluka Nyagali, maarufu Mdude Chadema, wametangaza kuendelea na nia yao ya kuitisha maandamano ya kupinga mkataba wa uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya DP World ya Dubai.

Vilevile, wametishia kugoma kuitikia wito wa Jeshi la Polisi kuwataka kuripoti katika kituo cha polisi kila baada ya siku saba pamoja na zuio la kutotoka nje ya Mkoa wa Mbeya wakidai kuwa mpaka sasa hawajui sababu za kuchukuliwa hatua hizo.

Wawili hao siku za hivi karibuni walikuwa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za uhaini. Walikamatwa Agosti 12 mwaka huu mkoani Morogoro wakiwa safarini kuelekea Dar es Salaam na kusafirishwa mpaka mkoani Mbeya.

Baadaye waliunganishwa na mwanasiasa maarufu, Balozi Dk. Willibrod Slaa, ambaye alikamatwa mkoani Dar es Salaam na kusafirishwa mpaka mkoani Mbeya.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kuripoti kwa mara ya kwanza katika kituo cha polisi tangu walipoachiwa kwa dhamana, wawili hao walisema nia yao ya kutetea rasilimali za nchi iko palepale.

Wakili Mwabukusi alisema wao tangu awali walikuwa na nia ya kutumia nguvu ya umma kupinga mkataba huo na mahakamani alikwenda kwa ajili ya kuwatetea wateja ambao walifungua kesi.

Alisema kwa sasa wanajiandaa kwa ajili ya kuratibu maandamano ya nchi nzima kupinga mkataba huo ambao alidai unataka kuifanya Tanzania kuwa koloni la Dubai.

"Kitendo cha sisi kukamatwa na kupewa kesi ambayo ilikuwa nzito hakiwezi kuturudisha nyuma, tunaendelea na nia yetu na ndani ya muda mfupi tutawatangazia Watanzania namna tutakavyoendesha maandamano hayo," alisema Mwabukusi.

Kuhusu kuripoti tena katika kituo cha polisi Agosti 28, mwaka huu kama ambavyo wanatakiwa na jeshi hilo, Wakili Mwabukusi alisema hawatatekeleza na kwamba jana ilikuwa siku ya mwisho kwao.

Wakili Mwabukusi pia alilitaka Jeshi la Polisi kuwarejeshea vifaa vyao, hasa simu na kompyuta ambavyo lilichukua baada ya kuwakamata ili waendelee na kazi zao.

Mdude alisema maandamano ya kutetea rasilimali za nchi ni haki ambayo ipo kikatiba na hivyo wao wataendelea nayo. Kwa sasa wanakusudia kuonana kwanza na Balozi Dk. Slaa ili wakubaliane namna ya kufanya.

Alisema watakapotaka kuanza maandamano hayo, watatoa taarifa kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya kuomba ulinzi huku akisisitiza hawaogopi kukamatwa tena.

Alisema mpaka sasa bado hawajui sababu ya kukamatwa kwao kwa maelezo kuwa kesi waliyokuwa wametajiwa awali ya uhaini haina dhamana kwa mujibu wa sheria.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha NCCR Mageuzi, James Mbatia, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kulishughulikia tatizo hilo la mgogoro wa Bandari kabla halijawa kubwa zaidi, akidai linachafua taswira ya nchi.

Alisema mgogoro huo kwa sasa umeligawa taifa ambapo zimeanza kutolewa kauli mbalimbali ambazo zingine ni za ubaguzi wa dini na wa Tanganyika na Zanzibar.

Pia alilishauri Jeshi la Polisi kuwarejeshea vifaa vyao kina Mwabukusi na Mdude ambavyo lilichukua baada ya kuwakamata, akieleza kuwa vifaa hivyo ndivyo wanavitumia katika kazi zao - simu na kompyuta mpakato.

# Wadaiwa kushikilia abiria na kudai fedha kwa ndugu

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA



JESHI la Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, linawasaka watu wanaodaiwa kuhusika na tukio la kumshikilia na kumpora, Sostensia John, wakitumia bajaji iliyokuwa ikitoka Mbagala kuelekea Mkuranga.

Watu hao wanadaiwa kufanya tukio hilo usiku wa kuamkia jana, wakitumia bajaji.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Protas Mutayoba, katika bajaji hiyo walikuwapo watu watano pamoja na dereva na kwamba aliyefikisha taarifa hizo ni mmoja wa abiria aliyeshikiliwa.

Kamanda Mutayoba alisema abiria huyo alilieleza Jeshi la Polisi kwamba baada ya kushikiliwa, aliachiwa baada ya kutoa fedha waliyohitaji watu hao.

Sostenesia alilieleza Nipashe kwamba alipanda bajaji hiyo akitokea Mbagala Misheni akiwa abiria watatu na dereva.

Alidai kuwa walipofika maeneo ya Kisemvule, bajaji dereva alisimamisha bajaji na alimwomba mmoja wa abiria (wa kiume) ashuke amnunulie sigara na alifanya hivyo na akaongezeka abiria mwingine wa kiume.

Kwa mujibu wa Sostenesia, waliendelea na safari na walipofika Mwanambaya, bajaji iliingizwa kushoto na dereva aligeuza akaondoka na kuwaacha.

"Nilihoji kwanini tunatoka barabara kuu tunaingia huku kwenye vumbi, kuna msafara au nini sikujibiwa badala yake tulishushwa wote tuliokuwa kwenye bajaji, dereva akaondoka na mimi nilifungwa kitambaa na kuanza kutembezwa hadi msituni.

"Waliokuwa wanafanya vitendo hivyo ni abiria niliokuwa nao kwenye bajaji, tulikwenda sehemu maarufu kama Shamba la Mwarabu na nilitakiwa kupiga simu kwa ndugu yangu yeyote atume Sh. 200,000 ndipo waniachie," alidai.

Sostenesia alisema alimpigia simu mjomba wake ambaye alituma fedha hiyo na walipoitoa, walitoa laini yake kwenye simu na kunpatia kisha wao wakabaki na simu na kumwelekeza njia ya kufika barabarani kupata gari.

Kwa kuwa alikuwa anaelekea, Mkuranga alifanikiwa kupata lifti kwenye gari iliyobeba pilipili hoho. Akasafiri usiku huo.


BIDCITY AUCTION & ESTATE SALES

House No. 44
Along Coca cola Rd
Mikocheni B
Opp. East Africa International School
Dar es Salaam - Tanzania

## NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**BID CITY AUCTION & ESTATE SALES LIMITED,** Kwa idhini tuliyopewa na **KCB BANK TANZANIA LIMITED, MAKAO MAKUU, DAR ES SALAAM,** tutauza kwa Mnada wa hadhara dhamana za wadaiwa zilizo kwenye jedwali chini, endapo watashindwa kulipa madeni wanayodaiwa ndani ya muda wa siku ishirini na moja (21) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Mnada utafanyika mahali zilipo dhamana hizo kama tarehe na muda ulivyoonyeshwa kwenye jedwali.

| | AINA YA DHAMANA | MAELEZO/SEHEMU ILIPO DHAMANA | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA | C.T No 86330 DAR, Kiwanja Namba 952, Kawe, Kinondoni, Ukubwa ni Mita za mraba 1030. | 11/09/2023, Kuanzia Saa 3:30 Asubuhi |
| 2 | NYUMBA | CT. No 49864, DAR, Kiwanja Namba 910, Kitalu "J" Mbezi Beach, Kinondoni, Ukubwa wa mita za mraba 1491 | 11/09/2023, Kuanzia Saa 6;30 Mchana |
| 3 | NYUMBA | C.T No 41791, DAR, Kiwanja Namba 26, Kitalu "B" Kijitonyama, Kinondoni, Ukubwa ni mita za mraba 440 | 12/09/2023, Kuanzia Saa 4:00 Asubuhi |
| 4 | APARTMENT | C.T No. 97632, DAR, Kiwanja Namba 3, Kitalu Namba 25A, Mwananyamala, Kinondoni, Ukubwa ni mita za mraba 489.4 | 12/09/2023, Kuanzia Saa 6:30 Mchana. |
| 5 | NYUMBA | C.T No. 81441, DAR, Kiwanja Namba 2050, Kitalu "B" Kimara Baruti, Kinondoni, Ukubwa ni mita za mraba 612 | 13/09/2023, Kuanzia Saa 4:00 Asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada endapo bei hiyo itakubaliwa na Benki na salio la 75% litalipwa ndani ya siku kumi na nne (14).
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio ndani ya siku 14, atakuwa amepoteza haki yake ya malipo ya 25% na dhamana itauzwa upya
3. Gharama zote kuhusu kubadilisha jina na umiliki wa dhamana zitakuwa juu ya mnunuzi.
4. Baada ya kukamilisha malipo yote ni jukumu la mnunuzi kumuhamisha mkazi/wakazi waliopo katika dhamana husika.
5. Dalali atawasilisha Benki bei iliyofikiwa katika mnada na Benki ina haki ya kukubali au kuikataa bei iliyofikiwa katika mnada.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi:**
**Bid City Auctions & Estates Sales Limited**
**House No.44 Mikocheni B, Coca Cola Road**
**Dar es Salaam**
**0713815100/ 0719000002/ 0758182468**
**adolf.mboya@bidcity.co.tz**

Phone: +255 712 759 377 +255 719 000 002 | Mikocheni B | House No. 44 Along Cocacola Rd | Opp. East Africa International School Dar es Salaam - Tanzania | www.bidcity.or.tz info@bidcity.com

RIPOTI MAALUM

# Mradi wa soko ulivyogeuka 'nyonya damu' kwa manispaa

**Na Jenifer Gilla**

UJENZI wa Soko la Bwawani umegharimu Sh. bilioni 1.2. Matarajio yalikuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni iingize Sh. 77,000 kwa siku kutokana na vizimba 154 vya soko, lakini sasa inaambulia 2,500 kwa siku.

Vilevile, halmashauri ilitarajia ikusanye Sh. milioni 3.3 kwa mwezi kutokana na kodi ya vibanda 33 vya soko hilo, lakini sasa inakusanya Sh. 700,000 toka kwa wafanyabiashara saba waliopo, vibanda (vyumba) 26 havina wapangaji.

Liliko soko hilo, ni katika Mtaa wa Bwawani, Kata ya Mwananyamala, wilayani Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, Km 4.3 kutoka makao makuu ya Manispaa ya Kinondoni na Km 6.7 kaskazini magharibi mwa Soko la Kimataifa la Kariakoo.

Ujenzi wa soko hilo lililozinduliwa Agosti 2021, ukitekelezwa kupitia Mradi wa Uboreshaji Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP), ulilenga kuboresha maeneo ya biashara na kusogeza huduma za kijamii kwa wananchi, lakini imekuwa kinyume. Miundombinu ya soko mingi haitumiki. Imekosa wateja.

Mwandishi wa habari hizi amebaini baadhi ya vyumba (vibanda) vilivyopaswa kuwa na bidhaa za soko, vinatumika kama malazi ya mafundi wanaoendelea na ujenzi wa soko hilo.

Vilevile, mwonekano wa barabara katika Mtaa wa Bwawani, liliko soko hilo, ni nyembamba, imezingirwa na makazi ya watu kiasi cha kutia shaka uwezekano wa magari ya mizigo na daladala kutumia njia hiyo.

**HASARA**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Manispaa ya Kinondoni, Aquilinus Shinduki, akitoa ufafanuzi kwa mwandishi wiki iliyopita, alisema soko hilo lina vizimba 154. Kati yake, vitano vina wapangaji wanaoendelea na biashara na kulipa ushuru wa Sh. 500 kwa siku.

Alisema kwa hali hiyo, manispaa inakusanya kodi ya Sh. 2,500 kwa siku badala ya Sh. 77,000, hivyo kupata hasara ya Sh. 74,500 kwa siku sawa na Sh. milioni 2.235 kwa mwezi.

Shinduki alibainisha soko lina vyumba 33 ambavyo wapangaji wake wanatakiwa kulipa kodi ya Sh. 100,000 kwa mwezi, lakini kwa sasa ni wapangaji saba ndiyo wamefungua biashara na kulipa kodi. Kwahiyo, wanakusanya Sh. 700,000 badala ya Sh. milioni 3.3, hivyo kuwa na hasara ya Sh. milioni 2.6 kwa mwezi.

"Ukipiga hesabu hapo, utagundua kuwa kwa mwezi serikali inakosa mapato ya Sh. milioni 4.835 (vizimba na vyumba). Sababu kuu ni wafanyabiashara waliojiandikisha kuchukua maeneo hayo kwa ajili ya kuendesha biashara, hawafanyi shughuli hizo na hawalipi malipo stahiki," alifafanua.

Alisema kuwa wakati soko hilo linafunguliwa mwaka 2021, mwitikio wa wafanyabiashara ulikuwa mkubwa na halmashauri ikawaamini na kuwapa maeneo, lakini kadri siku zilivyosonga, wanapungua.

**WAFANYABIASHARA**

Elizabeth Kayanga, mmoja wa wafanyabiashara wenye vizimba katika soko hilo, alisema kukosekana wateja ni sababu inayowasukuma wafanyabiashara kuondoka na kukimbilia kwenye maeneo mengine kutafuta wanunuzi wa bidhaa zao.

Elizabeth alisema wakati soko hilo linaanzishwa mwaka 2021, alichukua kizimba kwa lengo la kuuza nafaka kama mchele, unga, maharagwe, lakini hakukuwa na wateja. Kuna kipindi aliuza kilo moja katika kila bidhaa zake kwa wiki na wakati mwingine hakuuza kabisa.

Alisema aliamua kubadili biashara. Akawa anauza nguo za mtumba, lakini hali imeendelea kuwa mbaya. Amebadili mtindo wa biashara, akifafanua:

"Kwa sasa hapa sokoni ninakuja siku za Jumatano na Alhamisi tu. Jumatatu, Jumanne na Jumapili ninakwenda kuuza katika Mnada Kawe (Manispaa ya Kinondoni) na Jumamosi ninakuwa Biafra (Manispaa ya Kinondoni). Hata huko pia tunalipa ushuru, lakini angalau fedha ya kulisha familia unaiona."

Kukabiliana na changamoto za Soko la Bwawani, Elizabeth alisema walipeleka maombi manispaa itoe rukhsa daladala kupita katika eneo hilo na kupeleka magari yanayouza vitu vya jumla kama ilivyo katika Soko la Mabibo, ili kuchangamsha na kuvutia wateja, lakini hakuna kilichoamuliwa hadi sasa.

Mfanyabiashara wa miamala ya fedha katika soko hilo, James Lameck, alisema kuwapo masoko ya aina hiyo karibu na Soko la Bwawani, kunachangia kukosekana wateja kwa kuwa wanapata bidhaa katika masoko waliozoea, hivyo kuathiri biashara Bwawani. Ndicho kiini wafanyabiashara wengi kuondoka sokoni Bwawani.

Kama ilivyo kwa mtangulizi Elizabeth, Lamech anashauri serikali kuanzisha minada au kutoa rukhsa kwa magari kupeleka bidhaa sokoni huko kwa lengo la kuvutia wateja.

Mafanyabiashara wa Chakula



CAG Charles Kichere



Waziri wa Nchi ofisi ya Rais-TAMISEMI, Angellah Kairuki

sokoni huko, Asha Limamu, alibainisha kuwa wakati soko linaanzishwa, kulikuwa na wafanyabiashara katika vibanda na vizimba vyote, lakini kutokana na biashara kuwa ngumu, wengi waliondoka.

Ni hali ambayo Asha aliitaja inaathiri biashara yake kwa kuwa hakuna tena wa kumwuzia chakula. Analazimika kwenda nje ya soko kutafuta wateja, ilhali analipa fedha kwa ajili ya pango Sh. 100,000 kwa mwezi.

"Wakati soko linaanza, kwa siku nilikuwa ninapika kilo tano hadi sita za mchele na kilo tatu za unga wa ugali, lakini sasa ninapika kilo mbili za mchele na kilo moja ya unga wa ugali. Mauzo yangu yamepungua kutoka Sh. 50,000 kwa siku hadi 25,000," alisema.

Mfanyabiashara wa matunda na mboga, Magreth Matola, alisema kwa sasa anafika sokoni huko saa saba mchana. Anatumia muda wa asubuhi kutembeza biashara hiyo katika nyumba za watu ili apate fedha ya kukidhi mahitaji ya familia.

"Ukija hapa asubuhi, mboga na matunda vinakaa mpaka vinaoza, hakuna mtu anayekuja kununua. Watu wanakwenda kwenye masoko ya jirani na magenge ya mtaani walioyazoea. Serikali ilipaswa ihamishie watu wa kwenye hayo magenge katika soko hili," alishauri.

Mfanyabiashara wa pilipili sokoni huko, Shuwa Msaka, alibainisha kuwa awali alikuwa anauza nafaka, lakini alilazimika kubadili biashara baada ya nafaka hizo kuharibika kutokana na kukaa muda mrefu bila kupata wateja.

**KAULI YA MANISPAA**

Meneja wa Masoko Manispaa ya Kinondoni, Damaris Lujani, alikiri kupokea malalamiko ya biashara kuwa ngumu sokoni kutoka kwa wafanyabiashara hao. Aliyawasilisha kwa uongozi wa halmashauri.

Alibainisha malalamiko ya wafanyabiashara yanajumuisha mzunguko mdogo wa fedha kutokana na kukosa wateja, hali iliyosababisha baadhi yao kuishiwa mitaji na kushindwa kuendelea na biashara.

"Nilikusanya mapendekezo hayo na mengine na kuyapeleka manispaa. Kwahiyo, tunasubiri utekelezaji. Lakini hali iliyopo ni kuwa watu wametelekeza maeneo yao huku wakiwa wameyashikilia, hivyo serikali inakosa mapato," alisema.

Katika ufafanuzi wake kuhusu mikakati ya kukabiliana na changamoto zinazolikabili soko, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Manispaa ya Kinondoni, Shinduki, alisema manispaa itachukua hatua ili kulifanya soko kuwa na hadhi na kuvutia wateja ikiwamo kuangalia namna ya kutoa rukhsa kwa daladala kupita katika barabara hiyo.

Shinduki pia alisema wanataka kulibadilisha soko hilo liwe na bidhaa za nyumbani zaidi, ikiwamo vyombo, hivyo watafanya matangazo ili wale wenye sifa wawasilishe maombi halmashauri na kuanza biashara hiyo.

Pia alisema wanaandaa vikao na wafanyabiashara waliopo ili wasio tayari kuendelea na biashara, warudishe maeneo yao kwa manispaa, wapewe wengine wenye nia pia wataanzisha utaratibu wa kuingia mikataba ili kudhibiti wafanyabiashara kukimbia.

**JICHO LA UWAJIBIKAJI**

Meneja wa Miradi wa Taasisi ya WAJIBU, Moses Kimaro, katika mazungumzo na mwandishi jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, aliishauri manispaa ikae na wafanyabiashara hao kusikiliza kero zao na kuangalia namna ya kuzitatua ili soko lifanye kazi na kuingiza mapato serikalini.

Alisema kama hali sokoni ikiendelea kuwa kama inavyoshuhudiwa sasa, serikali itakuwa imefanya uwekezaji usio na tija kwa kuwa malengo ya mapato walioukuwa wamejiwekea yatakuwa hayajatimia.

Kimaro alisema hali hiyo pia itaathiri utekelezaji wa mipango ya manispaa na upatikanaji wa huduma za kijamii katika eneo hilo kwa kuwa lengo la kuweka soko hilo ni kusogeza huduma karibu na wakazi wa eneo hilo.

Kimsingi, kinachoshuhudiwa sokoni Bwawani kwa sasa, ni kutotekelezwa kwa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu miradi iliyokamilika, lakini haitumiki.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12, 2021, CAG Charles Kichere, mbali na mambo mengine, alipendekeza serikali ichukue hatua kuhakikisha miradi iliyokamilika ikiwamo ya masoko, itumike ili kufanikisha lengo la kutoa huduma kwa wananchi na kuingiza mapato serikalini.

Kimsingi, kinachoshuhudiwa sokoni Bwawani kwa sasa, ni kutotekelezwa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu miradi iliyokamilika, lakini haitumiki.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12, 2021, Katika ripoti hiyo, CAG anabainisha kwamba mabilioni ya shilingi yanatumika kutekeleza miradi ambayo ama haitumiki baada ya kukamilika au inatelekezwa katikati ya ujenzi na kutumia muda mwingi tofauti na ilivyopangwa.

Katika miradi iliyokamilika lakini haitumiwi na wananchi, CAG anasema katika ripoti yake kwamba iko katika halmashauri 30 ikiwa imetumia zaidi ya Sh. bilioni 7.68 bila kuwanufaisha wananchi.

Miongoni mwa sababu anazotaja za kutotumika miradi hiyo, ni ukosefu wa umeme, wataalamu wa kuendesha mifumo pamoja na idadi ndogo ya watumishi. Pia kutokuwapo mipango thabiti wakati wa uanzishaji wake.

Katika ripoti hiyo, CAG anaitaja Wilaya ya Lushoto, mkoani Tanga, ambako kulijengwa soko la mboga la Mnadani kwa Sh. bilioni 1.045, lakini halitumiki, sawa na hali ilivyo wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, ambako mabweni yalijengwa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Machame, lakini vitanda vya Sh. milioni 80 havikununuliwa hadi wakati wa ukaguzi.

CAG Kichere anapendekeza serikali ichukue hatua kuhakikisha miradi iliyokamilika ikiwamo ya masoko, itumike ili kufanikisha lengo la kutoa huduma kwa wananchi na kuingiza mapato serikalini.

Pia anashauri halmashauri kuongeza umakini katika uandaaji mipango ya miradi ili ikikamilika itumike na kuleta manufaa yaliyokusudiwa ili kupata thamani ya fedha, hasa kwa huduma zinazogusa maisha ya wananchi wengi katika sekta ya masoko, elimu na afya.

Alipotafutwa na mwandishi jana kuzungumzia suala hilo, Nteghenjwa Hosseah, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), alikiri kuwapo shida hiyo katika baadhi ya masoko, likiwamo la Bwawani.

Hatua wanazochukua, alisema Nteghenjwa wanatoa elimu kwa halmashauri ziwe na miradi inayokidhi haja za wananchi wa eneo husika, pia washirikishe wananchi kujua mahitaji yao na miradi wanayoitaka.

HABARI KITAIFA

# Mradi wa EBARR watatua changamoto za wafugaji

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR) unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF) na unatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Unatekelezwa katika wilaya za Kishapu (Shinyanga), Simanjiro (Manyara), Mvomero (Morogoro), Mpwapwa (Dodoma) na Kaskazini A (Unguja).

Lengo lake ni kuwezesha jamii, hasa za vijijini, kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Katika maeneo ya wafugaji ambako mradi unatekelezwa, kumekuwa na changamoto za migogoro kati ya wakulima na wafugaji inayotokana na uhaba wa maji na ukosefu wa malisho.

Changamoto nyingine ni mlipuko wa magonjwa yanayoshambulia mifugo, baadhi ya magonjwa hayo yakiwa ni matokeo ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Katika kukabiliana na changamoto ya magonjwa ya mifugo , mradi umeziwezesha jamii hizo za wafugaji kukabiliana au kupambana na magonjwa, hasa yale yanayoenezwa na wadudu kama kupe na mbung'o.

Kupitia mradi huo, kumejengwa majosho ya mifugo kudhibiti magonjwa hayo. Katika Wilaya ya Simanjiro, kumejengwa majosho mawili, Kishapu matatu na Mpwapwa mawili. Ni jitihada za kuziwezesha jamii za wafugaji kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Katika kuhakikisha migogoro kati ya wafugaji na wakulima inapungua, mradi umewezesha vijiji katika maeneo ya mradi kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi kwa vijiji 17, yaani shehia tatu upande wa Kaskazini A, Unguja; na vijiji 14 kwa upande wa Tanzania Bara katika wilaya za Kishapu, Simanjiro, Mpwapwa na Mvomero.

Mratibu wa Mradi wa EBARR, Dk. James Nyarobi, kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, anasema mipango hiyo shirikishi ya matumizi ya ardhi, imesadia kupunguza migogoro.

"Hii ni kwa sababu maeneo ya malisho yametengwa kwa ajili ya mifugo, maeneo ya kilimo kwa ajili ya shughuli za kilimo, misitu ya kijiji ambayo ni maeneo ya hifadhi, na pia maeneo ya makazi na matumizi mengine yameainishwa. Kupitia mpango wa matumizi ya ardhi, mradi umesaidia kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji katika maeneo ambako mradi unatekelezwa".

"Kwa mfano, katika Halmashauri ya Mpwapwa kulikuwa na mgogoro wa muda mrefu wa mpaka baina ya kijiji cha Ng'ambi na Kijiji cha Mbugani uliodumu zaidi ya miaka 15. Lakini kupitia mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi, ule mgogoro umetatuliwa na sasa vijiji hivi viwili vinaishi kwa amani, wakulima wanaelewa maeneo yao ya kufanya shughuli za kilimo, na wafugaji wanaelewa maeneo yao ya malisho na shughuli za ufugaji," anasema.

Dk. Nyarobi anaendelea kusema kuwa katika Wilaya ya Simanjiro, pia kulikuwa na mgogoro wa mpaka wa muda mrefu kati ya kijiji cha Langai na vijiji vya jirani. Lakini kupitia mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi, mgogoro huo ulitatuliwa kwa mipaka kubainisha maeneo ya malisho na maeneo kwa ajili ya shughuli nyingine.

Katika kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na matumizi mengine, malambo saba yamechimbwa katika Wilaya za Mpwapwa, Mvomero, Kishapu na Simanjiro na hivyo kupunguza tatizo la uhaba wa maji kwa ajili ya shughuli za mifugo, na kuwezesha kilimo cha umwagiliaji wa bustani za mbogamboga.

Mratibu wa mradi wa EBARR katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Godwin Everygist, anasema tatizo la kupeleka mifugo mbali kwa ajili ya maji sasa limepata ufumbuzi, na wakazi wa eneo la mradi wanaishukuru serikali kwa kuwaletea ahueni ya maji kwa ajili ya mifugo yao.

Mradi wa EBARR ulianza kutekelezwa mwaka 2018/19 na unategemewa kumaliza muda wake ifikapo mwaka 2024, yaani mwakani.





Baadhi ya wafanyabiashara wa vipuri wa eneo la Tandale Shule, Barabara ya Tandale Magharibi, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam, wakiwa wameegesha magari mabovu kwenye njia za waenda kwa miguu, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa wapita njia. **PICHA: KHADIJA KATEGILE/ TUDARCO**

# Bingwa wa moyo afariki dunia akitibiwa JKCI

**Na Christina Mwakangale**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. William Mahalu, amefariki dunia akiwa katika taasisi hiyo alikokuwa anapatiwa matibabu.

Prof. Mahalu ni miongoni mwa mabingwa watatu wa kwanza wa moyo nchini, walisomeshwa nje ya nchi miaka 1970 kwa ajili ya kutoa tiba za kibingwa nchini. Wengine ni Prof. Idrissa Mtulia na Prof. William Makene, aliyekuwa Daktari wa Rais wa Kwanza, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alisema Prof. Mahalu alifariki dunia usiku wa Agosti 20 mwaka huu, akiwa JKCI, alikokuwa anapatiwa matibabu.

"Ninasikitika kutangaza kifo cha Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi, Prof. William Rhys Mahalu kilichotokea jana usiku wa tarehe 20/08/2023 katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), alikokuwa anapatiwa matibabu. Bwana alitoa na Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe," alisema Dk. Kisenge.

Mei 9 mwaka huu, Prof. Mahalu, akiwa kwenye hafla ya utiaji saini ushirikiano baini ya JKCI na nchi ya Zambia na Rwanda kuboresha huduma za kibingwa kwenye nchi hizo, alisema:

"Ninachokishuhudia katika utendaji wa matibabu bobezi na ya kibingwa ni ndoto yangu kutimia. Wakati ninafikiria kuanzishwa kwa Taasisi ya Moyo ya JKCI, kila mmoja aliniona ninapoteza muda. Ninashukuru Mungu kunipa uhai na kushuhudia hiki leo (Mei).

"Kwa sababu wapo walionikatisha tamaa kwamba taasisi ya moyo sio kipaumbele, tujitahidi kufanya vitu wenyewe haijalishi kwa udogo gani. Upasuaji tufanye wenyewe," alibainisha Prof. Mahalu, enzi za uhai wake.

**ILIKOTOKA JKCI**

Unapozungumzia JKCI tangu kuanzishwa kwake hukosi kumtaja Prof. Mahalu kwa kuwa wazo la kuanzisha hospitali ya moyo nchini lilianza wakati wa Rais wa Kwanza, Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere miaka ya 1970, serikali



ilipowapeleka wataalam wawili nje ya nchi kwenda kusomea magonjwa ya moyo.

Walipohitimu masomo yao, wataalamu hao ambao ni Prof. Mtulia na Prof. Mahalu waliifanya Tanzania kuwa na madaktari bingwa watatu tu wa magonjwa ya moyo. Mwingine alikuwa William Makene, aliyekuwa daktari wa Rais Nyerere.

Baada ya takribani miongo minne ya kupanga na kuratibu, Tanzania ikafanikiwa kuwa na hospitali ya moyo inayotoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa wa ndani hata kutoka mataifa jirani.

Licha ya idadi hiyo ndogo ya wataalamu, ndoto ya kuwa na hospitali ya moyo iliendelea kudumu pamoja na kwamba haikutimia wakati huo, kwa sababu hapakuwa na miundombinu ya kufanyia kazi ikiwamo vifaa tiba.

"Miaka ya 1990 madaktari waliokuwapo na viongozi wa kitaifa walijadili upya na kuifanyia kazi mikakati ya kuanzisha kituo maalum cha matibabu ya moyo kitakachokuwa endelevu.

"Mikakati hii ilijumuisha uundaji wa vikosi kazi maalum ambavyo vilipewa jukumu la kupata uzoefu kutoka nchi nyingine juu ya uanzishaji na uendelezaji wa vituo vya matibabu ya moyo," alisema Mkurugenzi wa Fedha na Mipango wa JKCI, Agnes Kuhenga, alipohojiwa na jarida la taasisi hiyo mwaka 2021.

Alisema hatua hiyo ililenga kutatua changamoto zilizosababisha vituo vingi vya matibabu ya moyo barani Afrika kushindwa kuwa endelevu kwenye huduma hizo.

"Jitihada kuanzisha hospitali ya moyo ziliendelea na mwaka 2005/2006, chini ya uongozi wa awamu ya nne ya Rais Jakaya Kikwete, wataalamu 26 kutoka Idara ya Magonjwa ya Moyo ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), walipelekwa India kusomea magonjwa ya moyo.

Kuhenga anasema mikakati hiyo ilizaa matunda kwa kuwa mwaka 2008, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kushirikiana na Menejimenti ya MNH, ilianzisha Idara Maalumu ya Matibabu ya Moyo.

"Hatua hii ililenga kuimarisha huduma ambazo awali zilikuwa zinapatikana chini ya idara ya magonjwa ya ndani.

"Wataalamu hao waliokwenda kusoma India, walirudi nchini mwaka 2008 na kuanza kufanya kazi ya upasuaji wakitumia vitanda vinne vilivyokuwapo Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI).

"Wagonjwa waliofanyiwa upasuaji walilazwa katika wodi namba 12 ya Kibasila iliyoko MNH. Mipango ya kuanzisha hospitali ya moyo ilitimia baada ya ombi la Rais Kikwete kwa kushirikiana na Serikali ya Watu wa China, kufanikisha ujenzi wake," alisema Kuhenga.

Alibainisha kuwa China ilikubali kujenga jengo lililoko sasa kwa Sh. bilioni 13.6 na Serikali ya Tanzania ikatoa Sh. bilioni 13 kwa ajili ya kununua mashine, vitanda na vitu vingine muhimu na mwaka 2014 Kituo Maalum cha Matibabu ya Moyo kilizinduliwa.

"Kuhakikisha kinakuwa mamlaka kamili inayojitegemea, kwa matibabu ya moyo kuwa endelevu, Septemba 5, 2015, hati ya kuanzisha JKCI ilitiwa saini na ikaanza kufanya kazi kama taasisi inayojitegemea kuanzia Julai Mosi, 2016.

"Lengo la kuanzisha taasisi hiyo inayopokea wagonjwa kutoka mikoa yote nchini pamoja na nchi jirani za Burundi, Rwanda, Kenya, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Zambia, Visiwa vya Comoro, Zimbabwe na Malawi, ni kuimarisha na kuendeleza huduma za afya ya moyo na ustawi wa watanzania na majirani zao," alisema.

Prof. Mahalu alizaliwa Novemba 14, 1944.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili miradi TIC usaidie kupunguza tatizo la ajira

**NI** matarajio ya Watanzania wengi kuona miradi mingi inaposajiliwa nchini ni kusaidia kuwapatia ajira ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Miradi ni moja ya njia ya kupunguza tatizo la ajira iwe ya muda mfupi au muda mrefu, lakini mtu anapoipata humsaidia kumtoa mahali alipo na kumsogeza mbele.

Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), kimefanikiwa kusajili miradi 40 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 427. 4 kwa mwezi Julai pekee.

Miradi 40 ni mingi na inaweza kuwanufaisha vijana wengi nchini hasa wanaomaliza elimu ya vyuo vikuu.

Kwa mujibu wa taarifa ya kituo hicho uwekezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kuzalisha ajira mpya 7,689 kwa wazawa na wageni.

Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo unaongoza kwa kuwa na miradi mingi na kwa mwezi Julai ilisajili miradi 15 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 79.3, ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira 1,233.

Mkoa wa Dar es Salaam una idadi kubwa ya watu kutokana na watu wengi kuukimbilia kwa kupata urahisi wa kutafuta ajira.

Mikoa ambayo sasa inaonekana kuwa na idadi kubwa ya watu na ambayo ndiyo majiji kama Mwanza uliosajili miradi sita yenye thamani ya Dola milioni 24, unatarajiwa kuzalisha ajira 108.

Mkoa wa Mwanza ni kati ya majiji yenye umaarufu wa vivutio vya utalii hivyo pia kuwa sehemu ya kimbilio kwa vijana wengi kutafuta ajira.

Kwa miradi iliyosajiliwa katika mkoa huo, unaweza kupunguza idadi ya vijana wanaotafuta ajira.

Mkoa wa Pwani ambao pia una maarufu kutokana na rasilimali ulio nao, ulisajili miradi minne yenye thamani ya Dola milioni 10. 4 ambayo inatarajiwa kutengeneza ajira zipatazo 165.

Mkoa uliofuata kwa kusajili miradi ni Kilimanjaro uliofanikiwa kusajili miradi miwili yenye thamani ya Dola milioni 16.9 ambayo inatarajaiwa kutengeneza ajira 329.

Ilitaja mikoa mingine kuwa ni Lindi iliyosajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 4.5 ambao unatakiwa kutengeneza ajira 16, wakati Mtwara ikisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 21.7 na ajira 33.

Mkoa wa Iringa ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 4 na ukitarajiwa kutoa ajira 80, wakati Mkoa wa Rukwa ukisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 225 na ukitarajiwa kuzalisha ajira 510.


Mkoa wa Singida ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 10 ambao unatarajiwa kuzalisha ajira 110 na Geita ilisajili miradi miwili yenye thamani ya Dola milioni 2.5 ikitarajiwa kuzalisha ajira 108.

Mkoa wa Manyara ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 3.3 ukitarajiwa kutoa ajira 70 wakati Mkoa wa Mara ukisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 1.8 ukitarajiwa kuzalisha ajira 185.

Idadi ya mikoa iliyotajwa na TIC ambayo imesajili miradi hiyo ni mingi na ajira zitakazopatikana zitasaidia kuwainua baadhi ya watu watakaofanikiwa kupata ajira hizo.

Kwa watakaopata ajira hizo, ni fursa kwao ya kujifunza na kupata ujuzi ili hata itakapomalizika wawe na uwezo wa kujiajiri wenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Bajeti ya Wizara ya Afya ikomeshe ukosefu wa dawa

**VIPAUMBELE** vya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2023/24 ni kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa badala ya kutibu au kuponya ikiwamo kutoa chanjo, lishe bora, usafi na ulinzi wa mazingira.

Mbali na hivyo, vingine ni afya ngazi ya jamii, kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya umma katika ngazi zote, kusimamia upatikanaji wa dawa bora na udhibiti wa feki na pia kukabili wizi pamoja na vifaa tiba.

Kadhalika kipaumbele kingine ni upatikanaji wa vifaa vikiwamo vya tiba, vitendanishi na damu salama katika ngazi zote, bila kusahau huduma za mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Vifo hivyo vimo vya watoto wachanga, lakini wizara unakusudia kuboresha matibabu ya ubingwa na ubobezi ili kusogeza huduma hizo karibu na wananchi, kwa lengo la kuwapunguzia gharama za kupata matibabu hayo nje ya nchi, lakini pia kushughulikia changamoto za afya ya akili, yote yakitarajiwa kutekelezwa kwa bajeti ya Shilingi trilioni 1.2 ambazo wizara hiyo iliomba ziidhinishwe na bunge jijini Dodoma, kwenye mkutano wa bajeti uliomalizika Julai mwaka huu.

Katika vipaumbele vya wizara hiyo, nitajikita zaidi kwenye kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa. Pamoja na kwamba vipaumbele vyote vina umuhimu, lakini hili la upatikaji wa dawa lina uzito wake.

Imekuwa ni kama jambo la kawaida kukuta kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati za umma hazina dawa, jambo ambalo linaumiza watu wanaofika kupata huduma za afya.

Baadhi ya wananchi wamekuwa wakilalamikia hali hiyo,hasa pale wanapoambiwa hakuna dawa. lakini wanaelekezwa kwenda kununua katika duka lililo karibu na hospitali, kituo cha afya au zahanati.

Swali ni kwamba, inakuaje hospitali, kituo cha afya au zahanati ambavyo vyote ni vya umma vinakosa dawa, lakini duka lililo jirani linakuwa na dawa? Kwanini kuna hali hiyo?

Wakati mwingine wazee na wajawazito wanaotakiwa kupata huduma bure, nao hujikuta wakikosa kwa sababu hakuna dawa na wanaelekezwa kwenda kununua katika duka au maduka yaliyo jirani.

Vitendo hivyo viliwahi kuichefua serikali ikaelekeza maduka yote yaliyo karibu na huduma za afya za umma yaondolewe, baada ya kubainika kuwa kuna ujanja unafanyika na kusababisha ukosefu wa dawa.

Sasa kwa kuwa wizara imeamua kutoa kipaumbele kwenye upatikanaji wa dawa, basi ingemulika mianya yote inayosababisha hospitali za umma kukosa dawa lakini maduka ya jirani na hospitali hizo yakiwa na dawa.

Wakati mwingine ukosefu wa dawa unaweza kuchangia wananchi kusita kujiunga kwenye mifuko ya taifa ya bima kwa kuwa wanajua kuwa hata wakienda kupata huduma za afya wanaweza kuambulia patupu.

Mifuko hiyo kimsingi ni mizuri kwa sababu inasaidia kupunguza kero ambazo mtu anaweza kuzipata anapougua ghafla lakini akawa hana fedha, lakini kikwazo kinaweza kuwa ni hicho cha ukosefu wa dawa.

Hivyo ni vyema wizara ikafuatilia kujua uhaba wa dawa kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati za umma unatokana na nini ili kupunguzia wananchi adha wanayokutana nayo.

Huduma za matibabu katika hospitali za umma ni kulipia na pia ninaamini zina wataalam wazuri, hivyo, huduma hizo zingeboreshwa maeneo yote bila kusahau upatikanaji wa dawa.

Watu wengi wa hali ya chini wanapenda kupata huduma za afya katika hospitali za umma kwani zina gharama nafuu ila kikwazo wanachokumbana nacho ni kukuta hazina dawa.

Aidha, hata watu wazima wanaotakiwa kupata huduma za afya bure nao kumekuwapo na taarifa kwamba hukosa dawa kwa kuwa hazipo na kutakiwa kwenda kununua kitendo ambacho ni wazi wanaumia.

HABARI KITAIFA

## Mwanafunzi aliwa na mamba ziwani akiogelea

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MWANAFUNZI wa darasa la nne Shule ya Msingi Izinga wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Mathias Kikoso (10) amefariki kwa kuliwa na mamba wakati akiogelea kwenye Ziwa Tanganyika akiwa na wenzake.

Tukio hilo lilitokea Agosti 19, majira ya saa nane mchana wakati kundi la watoto hao wakiwa wamekwenda kuogelea ziwani.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Izinga, Edger Mkala, alisema kuwa watoto hao walikuwa wanaogelea ziwani, ghafla mamba aliyekuwa kwenye mawindo aliibuka karibu yao na kisha kumkamata mtoto huyo na kuondoka naye.

Alisema baada ya tukio hilo, watoto wenzake walitoka ziwani na kurudi kijijini bila kutoa taarifa kwa wazazi wao kwa hofu kuwa watachapwa kwakua walikwenda kuogelea.

Alisema ilipofika majira ya saa 1:30 ya usiku wazazi wa mtoto huyo walianza kumtafuta na walipowauliza watoto wanzake walieleza kuwa mwenzao alichukuliwa na mamba wakati wanaogelea ziwani.

"Baada ya taarifa hizo tulikwenda ziwani na kukuta nguo za mtoto huyo zikiwa pembeni ya ziwa na kwakuwa ilikua usiku hatukuweza kuutafuta mwili wa mtoto huyo na mpaka leo tumeweka msiba bila kuona maiti ya mtoto wetu," alisema.

Kwa mujibu wa maelezo ya Mwenyekiti huyo, tukio hilo ni la sita kijijini hapo, mwezi Aprili, mwaka huu mwanafunzi wa darasa la sita alipoteza maisha kwa kuliwa na mamba kijijini humo.

Siku za nyuma pia wavuvi wanne walipoteza maisha kwa nyakati tofauti kwa kuliwa na mamba hali ambayo inasababisha hofu kwa wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi ambazo ni uvuvi wa samaki.

Mkala alisema kuwa hivi sasa kuna ongezeko kubwa la wanyama hao kutokana na kuzaliana kwa wingi na kuiomba serikali kuwavuna kuwaepusha na tishio kwa maisha yao na kukwamisha jitihada za kujitafutia kipato kupitia uvuvi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Shedrack Masija, amekiri kutokea kwa tukio hilo na kuwataka wazazi kuwakataza watoto wao kwenda kuogelea ziwani ili kuepuka kuhatarisha maisha yao.

Alisema hivi sasa mkoani humo kuna ongezeko kubwa la wanyamapori baada za mamlaka za hifadhi kufanikiwa kudhibiti ujangili, wanyama wengi wameongezeka ikiwamo wakali na kutishia maisha ya wanadamu.

**Kwa mujibu wa maelezo ya Mwenyekiti huyo, tukio hilo ni la sita kijijini hapo, mwezi Aprili, mwaka huu mwanafunzi wa darasa la sita alipoteza maisha kwa kuliwa na mamba kijijini humo.**




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika Tanzania, Adam Mihayo, akizungumza wakati wa kongamano la wajasiriamali lililoandaliwa na benki hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya kuwapatia elimu ya biashara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TIC yasajili miradi itakayozalisha zaidi ajira 7000 nchini

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji nchini (TIC), kimefanikiwa kusajili miradi 40 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 427.4 kwa mwezi Julai pekee.

Kwa mujibu wa taarifa ya kituo hicho iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam, uwekezaji huo unatarajiwa kuzalisha ajira mpya 7,689 kwa wazawa na wageni.

Taarifa hiyo inaonyesha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo unaongoza kwa kuwa na miradi mingi na kwa mwezi Julai ilisajili miradi 15 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 79.3, ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira 1,233.

Taarifa hiyo ilitaja mkoa uliofuata kuwa ni Mwanza uliosajili miradi sita yenye thamani ya Dola milioni 24, inayotarajiwa kuzalisha ajira 108.

Taarifa hiyo ilisema Mkoa wa Pwani ulisajili miradi minne yenye thamani ya Dola milioni 10. 4 ambayo inatarajiwa kutengeneza ajira zipatazo 165.

Kwa mujibu wa taaifa hiyo, mkoa uliofuata kwa kusajili miradi ni Kilimanjaro uliofanikiwa kusajili miradi miwili yenye thamani ya Dola milioni 16.9 ambayo inatarajiwa kutengeneza ajira 329.

Ilitaja mikoa mingine kuwa ni Lindi iliyosajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 4.5 ambao unatarajiwa kutengeneza ajira 16, wakati Mtwara ikisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 21.7 na ajira 33.

Ilisema Mkoa wa Iringa ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni nne na ukitarajiwa kutoa ajira 80, wakati Mkoa wa Rukwa ukisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 225 na ukitarajiwa kuzalisha ajira 510.

Taarifa hiyo ilisema Mkoa wa Singida ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 10 ambao unatarajiwa kuzalisha ajira 110 na Geita ilisajili miradi miwili yenye thamani ya Dola milioni 2.5 ikitarajiwa kuzalisha ajira 108.

Mkoa wa Manyara ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 3.3 ukitarajiwa kutoa ajira 70 wakati Mkoa wa Mara ukisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 1.8 ukitarajiwa kuzalisha ajira 185.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



HABARI KITAIFA

# Anayedaiwa kuua wanawake wawili afikishwa kizimbani

**Na Steven William,** MUHEZA

MTUHUMIWA Salehe Ally (38), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, kujibu shtaka la mauaji ya wanawake wawili wa familia moja, wakazi wa Kijiji cha Mkanyageni kwa kuwakata mapanga.

Jana umati wa wananchi ulijitokeza katika viunga vya Mahakama ya Wilaya Muheza, kusikiliza shauri hilo lililofikishwa mahakamani humo kwa mara ya kwanza.

Tukio la mauaji ya wanawake hao wote wakiwa ni wa familia moja lilitokea Julai 21, mwaka huu katika kijiji cha Mkanyageni, wilayani Muheza.

Mtuhumiwa huyo amefikishwa jana katika mahakama hiyo na kusomewa shtaka lake mbele ya Hakimu Mkazi Msaidizi, Bahati Manongi.

Mwendesha Mashtaka wa Polisi katika mahakama hiyo Michael Msangawale, alidai kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo Julai 21, mwaka huu katika kijiji cha Mkanyageni.

Aliwataja wanawake wanaodaiwa kuuawa na mtuhumiwa huyo kuwa ni Mwanahawa Hatibu ambaye ni mke wa mtuhumiwa na Sauda Sofiani.

Mtuhumiwa huyo baada ya kusomewa mashtaka yake hakutakiwa kujibu lolote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka kisheria kusikiliza kesi za mauaji.

Hakimu Manongi aliahirisha kesi hiyo hadi itakapotajwa tena Agosti 31, mwaka huu.



Mtuhumiwa wa mauaji ya wanawake wawili katika kijiji cha Mkanyageni wilayani Muheza mkoani Tanga, Salehe Ally Miraji, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kusomewa shtaka linalomkabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya wilaya hiyo, jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mahakama kutoa uamuzi kisheria kesi walimu wanaodaiwa kuvujisha mtihani

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imetoa ahirisho la mwisho katika kesi ya walimu wanaodaiwa kuvujisha mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka 2022 na imeamuru upande wa mashtaka kuleta mashahidi, isipofanya hivyo mahakama itaamua kwa mujibu wa sheria.

Uamuzi huo wa mahakama umetolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Pamela Mazengo wakati kesi hiyo ilipokuja kwa ajili ya kusikilizwa lakini ilikwama baada ya upande wa mashtaka kudai jalada liko Polisi.

Wakili wa Serikali, Titus Aron alidai shauri lilikuja kwa ajili ya kusikilizwa, jalada limeitishwa polisi kwa ajili ya uchunguzi.

Akijibu, wakili wa utetezi, Nestori Mkoba, alidai shauri lina muda mrefu tangu upelelezi kukamilika, upande wa serikali kila wakifika mahakamani wanatoa sababu mbalimbali.

"Kwa upande wetu tumeweza kuwavumilia sana upande wa mashtaka, Julai 24, mwaka huu, shauri lilipokuja mara ya mwisho walisema wana mashahidi wawili ambao walipewa onyo, hadi mashahidi wamekuja mahakamani maana yake upelelezi umeshakamilika.

"Inakuaje leo wanasema jalada limerudishwa polisi kwa ajili ya uchunguzi, sisi tunaona upande wa mashtaka hawana juhudi za kuendelea na kesi hii," alidai Mkoba.

Wakili Aron akijibu, alidai shauri hilo hawawezi kuendelea nalo kwa sababu hawana jalada liko polisi, aliomba ahirisho la siku 14 ili waweze kuendelea na shauri.

Hakimu Mazengo baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili alisema ni kweli shauri ni la muda mrefu, aliungana na upande wa utetezi kama wanavyodai.

"Naunga mkono hoja za upande wa utetezi, kama hamtaleta shahidi tarehe inayopangwa mahakama itatoa uamuzi kwa mujibu wa sheria inavyotaka, hili ni ahirisho la mwisho," alisema Hakimu Mazengo.

Mahakama iliahirisha shauri hilo hadi Septemba 11, 12 na 13 mwaka huu kwa ajili ya kusikiliza ushahidi wa upande wa mashtaka.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni mwalimu Jacob Adagi, Joel Ngome, Lloyd Mpande, Reonard Ondieka, Patrick Chawawa, Theresia Chitanda, Elinami Sarakikya, Joyce Nkomola, Docras Muro na Alcherous Malinzi.

Inadaiwa kuwa kati ya Oktoba 2 hadi 12 mwaka 2022, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao walisambaza mtihani huo kupitia mtandao wa kijamii wa Whatsapp na Telegram na kusababisha kuvuja kwa watu ambao hawakuwa na mamlaka ya kuusimamia.

Inadaiwa pia katika tarehe hizo Mkoa wa Dar es Salaam, mshtakiwa Malinzi alitengeneza nyaraka za uongo kuonesha kuwa mtihani wa Taifa wa Darasa la saba wa somo la Uraia, somo la Maadili na Maalifa ya Jamii ni halali ilitolewa na Baraza la Taifa la Mitihani wakati akijua si kweli.

## Waganga tiba asili waonywa kukataza wagonjwa kutumia dawa za hospitali

**Na Stevie chindiye,** TUNDURU

MRATIBU wa tiba asili, kifua kikuu na ukoma wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, Dk. Mkasange Kihongole amewataka waganga wa tiba asili kuachana na tabia za kuwazuia wateja wao kuendelea na matumizi ya dawa za hospitali ili kuwasaidia wateja wao kupata nafuu na kupona magonjwa yanayowasumbua.

"Endelea kuwatibu ila tunakuomba usiwazuie kuendelea na dawa za kitaalamu ili kulinda afya zao," alisisitiza Dk. Kihongole.

Pia, aliwaasa waganga wote wa tiba asili wilayani humo kutoa huduma hiyo kwa kufuata maelekezo ya kisheria yanayotolewa na serikali ikiwa ni pamoja na kuwa na vibali vinavyo waruhusu kufanya shughuli hiyo.

Alisema hayo wakati akiongea na wagonjwa walio kusanyika kufuata tiba asili kwa mganga aliyetambulika kwa jina la Said Daudi Mohammed Simba maarufu kwa jina la Bibi Naweza, anayefanya shughuli hiyo katika kitongoji cha Kigamboni, Kijiji cha Semeni.

Kihongole alisema baada ya ofisi yake kupata taarifa za mganga huyo walianza kufanya ufuatiliaji na kutuma watu ambao walienda na kujifanya wagonjwa na kutibiwa.

"Katika ufuatiliaji huo, kwa bahati mbaya walipata taarifa za kushtua baada ya baadhi ya wateja wake kutamba kuachana na matumizi ya dawa za hospitali wakiwamo wagonjwa wanaotumia dawa za kufubaza maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU)," alisema.

Pia waligundua baadhi ya makopo ya dawa hizo yakiwa yametupwa katika eneo la pori jirani na kilinge cha kutolea dawa zake.

Akizungumzia mapokeo ya maelekezo hayo, msaidizi wa mganga huyo, Salum Mtingala, alisema mganga huyo alianza kazi Februari 28, 2023 na tangu aanze kutoa huduma hiyo, kwa siku uhudumia zaidi ya watu 500.

Alisema eneo lao limekuwa likifurika watu hali ambayo inaonesha uwapo wa uhitaji wa msaada wa miundombunu ya kitaalamu ili kuwalinda wateja wao na milipuko ya magonjwa.

Wakizungumzia maelekezo ya kufuatilia vibali, Mtingala na mke wa mganga huyo, Shamshia Mohamed, walisema kuwa wameyapokea maelekezo hayo na wapo tayari kufanya ufuatiliaji.


Mtendaji wa kijiji hicho, Emil Njovu, alikiri kushuhudia maelfu ya wananchi wanaomiminika kuelekea kwa mganga huyo.

Wakitoa ushuhuda kwa nyakati tofauti, baadhi ya wagonjwa hao, Juma Makumbusya, aliyempeleka binti yake alisema kwa sasa anaendelea vizuri.

"Nimezunguka sana hospitali na kwa waganga wa tiba asili lakini mgonjwa wangu alikuwa haoneshi mabadiliko kama ninayo yaona baada ya kutumia dawa za bibi Naweza," alisisitiza Makumbusya.

Aliyedai kunywa dawa za bibi Naweza kwa majaribio na kupona maambukizi ya VVU na kuacha dawa kwa zaidi ya mwezi, Hadija Mkwendaga, alisema baada ya kunywa dawa hizo alienda katika zahanati ya a Kijiji cha Mtina na vipimo kuonesha kuwa hana maambukizi ya ugonjwa huo.

Shuhuda mwingine aliyedai kupona tezidume baada ya kutumia dawa hizo, Harid Mohammed, alisema tiba asili imemsaidia na sasa ameondolewa mpira aliokuwa amewekwa kwa ajili ya kumsaidia kutolea haja ndogo.



## CCM Arumeru yaridhishwa utekelezaji ilani 2020/25

**Na Allan Isack,** ARUMERU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, kimeridhishwa na utekelezaji wa ilani ya chama hicho, kwa ujenzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Arusha wilayani humo.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Arumeru, Noel Severe, alithibitisha jana kuridhishwa na utekelezaji wa ilani ya chama hicho kwenye halmashauri hiyo wakati wa uzinduzi wa jengo la maabara ya masomo ya sayansi katika Shule ya Sekondari Oldonyowas.

Ujenzi wa mradi wa maabara hiyo ulitekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwenye shule hiyo.

Kadhalika, alisema serikali imetoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kisekta katika halmashauri hiyo.

Severe alisema baada ya serikali kutoa fedha hizo za ujenzi wa miradi ya maendeleo ina matarajio makubwa itakwenda kuleta matokeo chanya kwa wananchi.

Aidha, alisema ameridhishwa na ujenzi wa miradi hiyo kwa kuwa utekelezaji wake umezingatia viwango vya ubora unaoendana na thamani halisi ya fedha zinazotolewa na serikali kwa kuwa ni utekelezaji wa ilani ya chama ya mwaka 2020/2025.

Alisema: "Ninawapongeza kwa kazi nzuri mnazozifanya. Pia, kwa wataalamu kwa usimamizi wa miradi ya maendeleo, miradi ni mizuri imezingatia viwango na ubora kulingana na thamani ya fedha na imeleta matokeo chanya ya utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wananchi".

Aliongeza: "Nidhahiri kwa kazi zilizofanyika tunamuunga mkono Rais Dk.Samia katika utekelezaji wa ilani ya chama ya mwaka 2020/2025. Hakika ninawapongeza sana hasa wataalamu na wananchi kwa ujumla". Pia, alitumia fursa hiyo kutoa pongezi kwa wananchi kwa ushiriki wao kwa utekelezaji wa miradi hiyo kwa kujitolea nguvu kazi kwenye shughuli za ujenzi, pamoja na usimamizi wa miradi iliyojengwa kwa kuwatumia mafundi jamii.

Kadhalika alitoa rai kwa wanafunzi kusoma kwa bidii akisema serikali itahakikisha kila mwanafunzi anapata elimu ya msingi kuanzia darasa la awali mpaka kidato cha nne bila malipo.

Alisema awali jamii za kimaasai watoto wa kike hawakupata fursa ya kupata elimu ya sekondari kutokana na mila na desturi na uchache wa shule kwa nyakati hizo, lakini kwa sasa serikali imejenga shule za sekondari kila kata na kutoa fursa kwa kila mtoto kupata nafasi ya kujiunga na masomo ya sekondari.

Alisema: "Niwatie moyo wasichana, someni kwa bidii, wanawake mnaweza,hakikisheni mnatumia fursa hii adhimu ili kufikia ndoto zenu, tunatarajia kupata wataalamu wa fani mbalimbali na viongozi wengi wa ngazi tofauti".

Mradi wa ujenzi wa jengo la maabara mbili za somo la fizikia na jiografia, umetekelezwa kwa Sh.milioni 99.7 fedha kutoka TASAF.

# Malecela awataka Watanzania kuepuka kugawanywa kidini

**Na Mary Mosha,** SAME

WAZIRI Mkuu Mstaafu, John Malecela ametoa hadhari kwa Watanzania kutokukubali kugawanywa kwa misingi ya ukabila, dini, ukanda wala bandari, badala yake waongeze ushirikiano na kudumisha amani iliyopo.

Aliyasema hayo jana wilayani Same mkoani Kilimanjaro wakati akizungumzia utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kusema kuwa upo umuhimu wa kila mtanzania kujitambua na kusimamia amani ya nchi.


Alisema endapo watashindwa kuwagawanya Watanzania wanaweza kuwatumia viongozi wa dini ambao kwa sasa kuna baadhi yao hawatekelezi majukumu yao vyema.

"Viongozi wa dini kama mkiona serikali kuna vitu haifanyi vyema waiteni waelezeni, waonyeni na vitu vyote vitaenda sawa, badala ya baadhi wanavyofanya kwa sasa kusimama kwenye mimbari na kusema hayo wanayoyasema ni sehemu ya kuligawa taifa," alisema Malechela na kuongeza:

"Mimi nitoe rai kwa Watanzania kuacha kugawanywa kwa misingi ya udini, hapo nyuma ilisimama misingi ya ukabila tukaishinda, lakini kwa sasa tunaweka dini, hili tusipokuwa makini itatugawa".

Alisema hivi sasa baadhi ya watu wanasema mkataba wa bandari unaumiza Watanzania lakini hawajawahi kuusoma wala kusikia mtu akiusoma.

Alisema hali hiyo ni mbaya hasa kwa wasomi, akiwataka watu hao wausome mkataba huo na kuuelewa, kama kuna matatizo wayaseme ili yarekebishwe na kuleta matokeo chanya kwa taifa.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Puma Energy na Mkurugenzi Mwenza wa Kampuni ya mafuta ya Trafigura, Hadi Hallouche, baada ya mazungumzo Ikulu ndogo jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Miongoni mwa mambo waliyojadili ni biashara ya hewa ukaa na gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Wengine ni Mkurugenzi wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah (kulia) na Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali kujenga matawi ya vyuo vikuu mikoani

**Na Oscar Assenga,** PANGANI

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatarajia kujenga matawi 14 vya vyuo vikuu kwenye mikoa ambayo haina vyuo vikuu ukiwamo Mkoa wa Tanga.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa kampeni ya "Niache Nisome" iliyoandaliwa na Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Zainabu Abdallah kwa kushirikiana na Mbunge wa Pangani (CCM) Jumaa Aweso.

Kampeni hiyo ambayo ilianzishwa na viongozi hao kwa lengo la kuhamasisha vijana wilayani humo kusoma kwa bidii hatua inayosababisha kukuza kiwango cha elimu wilayani humo.

Alisema chuo ambacho kimeanza mchakato wa kujenga tawi lake ni Chuo Kikuu Mzumbe ambapo inatajwa kwamba uwepo wake utawawezesha wakazi wa mkoa huo waliokuwa wakienda mikoa mengine kupata elimu ya juu ikiwemo kwenye chuo hicho kunufaika.

"Nimefurahishwa na ubunifu huu ambao mmeufanya hapa Tanzania kwa kweli ni jambo zuri na la kuigwa mfano kwa mustakabali wa elimu, lakini niwaambie Rais Samia Suluhu amekwisha kutuelekeza kujenga matawi 14 ya vyuo vikuu kwenye mikoa mbalimbali ambayo haina vyuo na Tanga nanyi mtanufaika na mpango huo" alisema Profesa Mkenda.

Kadhalika, alimsifia Mbunge wa Pangani, Jumaa Aweso akisema ni mtu muungwana na amekuwa akifuatilia suala la kutaka mkoa huo uwe na chuo kikuu.

Alisema hivyo kutokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu ya kutaka kuwepo na kampasi 14 kwenye mikoa ambayo haina vyuo vikuu, Tanga agizo hilo linakwenda kutekelezwa.


Kauli ya Waziri Mkenda ilitokana na ombi lililotolewa na Mbunge wa Pangani, Jumaa Aweso ambaye alimuomba Waziri huyo kuangalia uwezekano wa chuo kikuu kujengwa mkoani Tanga.

Alisema kwamba wakiwa na chuo kikuu mkoani humo watakaweze kutoa fursa kwa wanafunzi kusoma lakini kukuza uchumi kutokana na uwepo wa mzunguko ambao utakuwa chachu ya maendeleo.

Akizungumza katika kampeni hiyo, Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Madaraka, Elizabeth Chawinga, alisema kwamba wameamua kushiriki kama wadau wanaochangia madawati, madarasa na kompyuta na wanawafadhili wanafuzi kwenda kusoma kidato cha tano, sita na vyuo vikuu.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambaji Maji kutoka Tanga UWASA, Mhandisi Rashid Shabani, alisema Tanga Uwasa imeshiriki kwenye shughuli hiyo kama wadau wakubwa wa utoaji wa huduma ya maji wilayani Pangani.

Alisema katika bajeti zao za kila mwaka wamekuwa wakitenga fedha kuchangia elimu na katika kampeni hiyo walichangia Sh. milioni moja kwa ajili ya kutoa zawadi kwa vijana waliofanya vizuri kwenye shule ya msingi na sekondari.



# Wanaoishi na VVU waanza kutambuliwa kwa mfumo

**Na Timothy Itembe,** MARA

WAVIU 3,799 kati ya 63,000 wanaotumia dawa za kupunguza makali ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) katika mikoa ya Kanda ya Ziwa wamesajiliwa katika mfumo wa alama za vidole.

Ni utambuzi uliofanyika ndani ya wiki mbili kufikia Agosti 15 mwaka huu kwa Watu wanaoishi na VVU (WAVIU) uliofanywa na Amref.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mkazi Amref Afrika Tanzania, Dk. Florence Temu wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa hivyo katika mikoa ya Mara, Simiyu na Tanga iliyofanyika katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tarime hivi karibuni.

"Wagonjwa wetu hao wanaendelea kutumia mfumo huu wa kisasa wa utambuzi wa vidole hali inayoongeza ufanisi katika utambuzi wa wagonjwa wa VVU, utunzaji sahihi wa takwimu katika kitengo cha utunzaji na matibabu yake,"alisema Dk. Temu.

Dk. Temu alisema kuwa teknolojia hiyo inalenga kutatua changamoto ya utambuzi wa kawaida wa wagonjwa wapya na wazamani pamoja na utunzaji sahihi wa takwimu kama vile makosa na urudiaji wa usajili wa mteja.

Mkurugenzi Mkazi wa Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Marekani (CDC), Dk.Mahesh Swaminathan alishukuru serikali pamoja na ufadhili wa PEPFAR kupitia CDC Tanzania na mdau wake Amref Health Africa kwa kuwa mstari wa mbele katika kuboresha sekta ya afya kupitia miradi mbalimbali.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa Mara, Dominicus Lusasi alisema tangu kuanzishwa kwa mradi, Amref Tanzania imekua ikishirikiana na Wizara ya Afya na uongozi wa afya mkoa katika kuboresha shughuli za tathmini na ufuatiliaji, kuboresha mifumo ya takwimu na taarifa katika vituo vinavyopewa ufadhili katika Mkoa wa Mara.



Mchungaji wa Kanisa la Hosana Pentecost la Kambarage, Manispaa ya Shinyanga, Anjelina Kapaya (kulia), akikabidhi vifaa vya shule vikiwamo madaftari, sare, kalamu, soksi na mabegi kwa wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu, vilivyotolewa na Taasisi ya Nancy Foundation juzi. Wa pili kulia ni Ofisa Elimu Taaluma wa Manispaa hiyo, Wingwila Kitila. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Ahukumiwa jela siku 30 kwa kuvunja televisheni

**Na Remmy Moka,** SAUT

MKAZI wa Bujingo wilayani Ilemela, Paul Lukasi (27) amehukumiwa kwenda jela mwezi mmoja na faini ya Sh. 400,000 baada ya kukutwa na hatia ya kuvunja duka na kuharibu televisheni.

Shtaka hilo lenye usajili wa namba 99/2023 ilisomwa na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Ilemela, Nemi Sango Bulemo baada ya mtuhumiwa kukuwa na kosa la kuharibu mali ya Magreth John aliyevamiwa akiwa dukani kwake.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Bulemo alisema mtuhumiwa huyo alivamia duka la Magreth John majira ya saa nne asubuhi Julai 13 mwaka huu na kuvunja televisheni yenye thamani ya Sh.400,000 kwa kutumia jiwe.

Mshtakiwa huyo alikili kosa na kudai kuwa alikuwa amelewa wakati akifanya tukio hilo na kuiomba Mahakama impunguzie adhabu kwani hana sehemu maalumu ya kuingizia kipato chake na kuipata fedha hiyo.

Nae Mlalamikaji Magreth John(47), aliiomba Mahakama hiyo kumsaidia kupata fedha hizo kutokana na mtuhumiwa kumpa vitisho vya mara kwa mara kabla ya kufikishwa mahakamani hapo.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Bulemo, alisema alitoa adhabu ya kwenda jela mwezi mmoja na kulipa faini hiyo baada ya kifungo kumalizika mshtakiwa atatakiwa kulipa kiasi cha Sh.400,000 kutoka na thamni ya runinga ya malalamikaji.

Aidha, alisema hukumu hiyo itakuwa fundisho kwa wote wanatekeleza matukio mbalimbali katika jamii kwa kisingizio cha ulevi na kuitaka jamii kuacha tabia za kuchukua maamuzi bila kufikilia.

# Wananchi wamtwisha 'zigo' waziri ujenzi zahanati

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

WAKAZI wa Kata ya Ulewe Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wamemtwisha jukumu Naibu Waziri OR-Tamisemi, Deogratius Ndejembi kukamilisha ujenzi wa zahanati waliyoijenga, ili kuokoa maisha ya wajawazito na watoto wachanga.

Waliliwasilisha ombi lao hilo juzi katika mkutano wa hadhara uliotishwa na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, katika Kijiji cha Bugomba 'A' uliolenga kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi katika sekta ya elimu, afya, maji, kilimo na barabara.

Mmoja wa wakazi hao, Meki Pilipili alisema ukamilishaji wa zahanati hiyo umechukua muda mrefu tangu walipokamilisha boma lake na walichangishana Sh. 1,500 kila kaya na sasa wameanza kukata tamaa juu ya kukamilika kwake.

Alisema kwa sasa huduma za matibabu wanazipata katika Zahanati ya Nyalwelwe iliyopo umbali wa kilometa saba ndani ya kata, hali iliyowaibua na kumuomba Naibu Waziri huyo kuhakikisha analisimamia hilo na ujenzi wake unakamilika na kuanza kutoa huduma.

Naye Haruna Sumuni alisema wajawazito wengi wanalazimika kutohudhuria kiliniki kutokana na umbali huo, wakati mwingine wanalazika kufika na kujiandikisha kwa kupata kadi pekee na kwenda siku ya mwisho ya kujifungua.

Alisema wakati mwingine wajawazito wanakwenda siku ya mwisho kujifungua na hali hiyo imekuwa ikitishia usalama wa mama na mtoto tumboni.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani alisema amekuta jimboni kwake kuna maboma ya zahanati 26 zinazohitaji kukamilishwa na kufanikiwa kupata zaidi ya Sh.milioni 550 ambazo zilikamilisha maboma 14 kati ya hayo 11 yanatoa huduma.

Alisema ili boma hilo liweze kukamilika linahitaji kiasi cha Sh. milioni 100 na vifaa tiba vyake.

Alisema walipokea Sh. bilioni 3.4 na kujenga Hospitali ya Wilaya ambayo imekamilika na inatoa huduma kwa wananchi, kwamba walinunua vifaa tiba vya kisasa vya Sh. 500 na sasa wagonjwa hawasafiri tena umbali mrefu kutafuta matibabu katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama kama ilivyokuwa hapo awali.

Naibu Waziri OR-Tamisemi, Deogratius Ndejembi aliwaahidi wananchi hao kutafuta fedha hizo na kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo ili kuunga mkono jitihada za wananchi.

Alisema mwaka wa fedha uliopita serikali ilitoa Sh. bilioni 117 za kujenga vituo vya afya 234 nchi nzima na Wilaya ya Ushetu ilipata fedha hizo.

Alisema, kila mwezi serikali imekuwa ikitoa Sh. milioni 134 kila hospitali za wilaya kwa ajili ya ununuzi wa dawa na hakuna malalamiko kutoka kwa wagonjwa juu ya ukosefu wa dawa au kuambiwa wakanunue katika maduka ya nje.

Alisema endapo kuna wagonjwa wanakosa dawa basi watoe taarifa ili hatua zichukuliwe.

Ndejembi alisema serikali imetenga Sh. bilioni 919 za ununuzi wa magari ya wagonjwa na hospitali ya halmashauri hiyo itapata magari mawili na moja kwa ajili ya Mganga Mkuu ili kuhakikisha anakagua vema vituo vya afya na zahanati.



Ukurasa 12

Ukimnyonyesha ipasavyo ndivyo unavyomwepushia kifo, udumavu



Ukurasa 13

Yasiyowezakana visiwani yanapoanza kushuhudiwa

Nipashe TESA

Jumanne Agosti 22, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

Ni wakati wa kutafakari vijana watakavyotumika kunufaisha taifa

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Mabinti wanaorejea darasani baada ya uzazi wana haya...

WANAFUNZI waliokatisha masomo kutokana na ujauzito ambao sasa wamerejea darasani, wanaposhangilia nuru ya kutimiza ndoto zao, wanatoa ya moyoni kwa serikali.

NI mabinti wanaosoma katika kituo cha Tumbi Sekondari mkoani Pwani, ambao pamoja na kuishukuru serikali na kuhimiza wengine wenye changamoto kurejea tena masomoni wana maombi kadhaa kuanzia vitambulisho na mabweni.

Wanasema pamoja na kusoma bila gharama serikali ikibeba jukumu hilo, wanaiomba kuwasaidia waruhusiwe kutumia vitambulisho kama ilivyo kwa wanafunzi wengine ili walipe nauli ya wanafunzi.

Wanasema ni kutokana na gharama kubwa za nauli baadhi yao wanakatisha masomo kwa mara nyingine kwa kukosa pesa wanatakiwa kulipa kama abiria watu wazima.

"Wapo baadhi ya wanafunzi wanaishi mbali na vituo na uwezo wa wazazi kumudu gharama za nauli ni mdogo na hivyo hukwama kuendelea na masomo pamoja na kuwa na nia ya kurudia tena kukamilisha masoma," anasema binti jina tumelihifadhi.

"Umbali kwa baadhi yetu pia umekuwa chanzo cha wengine kupata mimba kwa mara nyingine kutokana na kukosa mahitaji na hivyo kuingia kwenye mitego mingine jambo ambalo linaendelea kutuweka njiapanda na kushindwa kutimiza ndoto zetu,"anaeleza.



Ofisa Elimu Mkoa wa Pwani Sara Mlaki.

Akizungumza kwa niaba ya wengine, anaiomba pia serikali kuwajengea mabweni kwenye vituo ili wasichana wakae shuleni na kuachana na adha ya kusafiri umbali mrefu na kuewaepusha na vishawishi.

Wanashukuru kuwapo kwa fursa hiyo na kuwataka wenzao walioko shuleni kuzingatia masomo na kuepuka kujikita kwenye makundi na mitandao ya jamii ambayo imekuwa chanzo cha baadhi yao kupata ujauzito wakiwa masomoni.

**WASIMULIA MACHUNGU**

Mmoja wa mabinti hao anasema baada ya kupata mimba alirejea nyumbani huku akijutia alichokifanya alipowaona wasichana wengine aliokuwa akisoma nao wakiendelea na masomo na kufanya vizuri darasani.

Anasema alijuta na kuomba msamaha kwa wazazi wake ambao walimlea na alipojifungua walianza kutafuta shule ili aendelee na masomo kama alivyoomba, baada ya mtoto wake kutimiza miaka miwili alipata nafasi kwenye Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kituo cha Tumbi Sekondari.

Kuanza kwake masomo ni moja ya malengo yake aliyoyaweka kufikia ndoto ya kuwa daktari na hivyo kujituma na kuuliza maswali mara kwa mara kwa walimu darasani ndicho anachofanya.

"Wapo wazazi na ndugu wanashindwa kutoa nafasi ya pili kwa watoto wao na hivyo msichana kushindwa kuishi kwenye ndoto zake kwasababu ya mimba jambo ambalo kwangu siliamini, imani yangu ni kwamba ukianguka unaweza kusimama tena na kupambania malengo yako" anasema binti mmoja.

Mwanafunzi mwingine anaeleza kuwa baada ya kupata mimba alifukuzwa nyumbani na baba yake, akalazimika kukimbilia kuomba hifadhi kwa mjomba ambaye alimlea hadi alipojifungua.

Anasema baada ya mtoto wake kukuwa aliomba kuendelea na masomo na shangazi yake anayeishi Kibaha alimsafirisha kutoka Njombe kwa ajili ya kuanza masomo kwa mara nyingine.

Anasema haikua rahisi kwa ndugu akiwemo baba yake kuelewa malengo yake lakini kwakuwa aliamua na kujutia alichofanya alitumia nafasi hiyo kusoma kwa bidii na yeye pamoja na wengine wanatarajia kufanya mtihani wa kidato cha nne mwaka huu.

Mratibu wa kituo cha Tumbi Sekondari, Getrude Mvungi, anasema mfumo huo umewasaidia wale ambao walikata tamaa ya kuendelea na masomo sasa wamebadilika.

Changamoto ya baadhi yao kukosa nauli nayo inaelezwa na mratibu kwamba inachangia utoro na kurudi nyuma, lakini pia wapo wazazi ambao wanatamani watoto wao waendelee na masomo lakini mwitikio unakosekana kwani hawana mwamko.

"Kipo kikwazo pia cha mawasiliano duni kati ya wazazi, walezi na walimu, watoto wakishaanza masomo malezi yanaachwa kwa walimu pekee, jambo ambalo limesababisha baadhi ya wanafunzi kupata mimba kwa mara ya pili na kukatisha masomo,"anaeleza Getrude.

Ofisa Elimu Mkoa wa Pwani Sara Mlaki anasema kuanzia mwaka 2021 na 2023 wanafunzi wa kike 163 waliokatisha masomo baada ya kupata mimba walirudi shuleni.

Sara anaeleza kuwa wanafunzi hao 42 ni wa mwaka 2021 hadi 2022 wakati 121 ni wa kuanzia mwaka jana hadi sasa na kwamba wapo ambao wanasoma kwenye vituo pamoja na watoto wao.

Anaongeza kuwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima wanafuatilia na kuhakikisha kuwa waliokatisha masomo kwa mimba wanafikiwa.

Katika kupambana suala la mimba shuleni, Sara anaeleza kwamba mkoa huo una mikakati

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

MAZIWA YA MAMA

# Ukimnyonyesha ipasavyo ndivyo unavyomwepushia kifo, udumavu



ILI mtoto akue kiakili na kimwili ni lazima anyonyeshwe kwa miezi sita bila kupewa chochote hata maji ya kunywa. Na kwamba, kwenda kinyume na maelekezo hayo ni kumsababishia mchanga udumavu na afya duni.

Mkoani Shinyanga kukosekana elimu na ufahamu sahihi wa kunyonyesha kwa wanawake kunaelezwa kuwa kunachangia kwa kiasi kikubwa tatizo la udumavu kwa watoto, anasema Ofisa Lishe wa Mkoa Yusuph Hamisi,.

Baadhi ya wanawake mkoani Shinyanga bado hawana elimu hiyo ya unyonyeshaji na kusababisha tatizo la udumavu unaotokana na unyonyeshaji duni kwa watoto kuendelea, anaongeza na kukiri kuwa kinamama bado hawana elimu sahihi, anasema katika mahojiano na Nipashe, kuhusu changamoto na mafanikio ya Wiki ya Uhamasishaji mkoani humo.

Kwa mujibu wa utafiti wa taifa wa masuala ya afya na lishe ya mwaka 2022, tatizo la udumavu kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano Shinyanga unatajwa kuwa na asilimia 27.5 ambazo zinamaanisha kuwa watoto takribani 28 kwa kila watoto 100 wameathirika na udumavu huo, wakati ukondefu mkoa unafikia asilimia 4.3.

Hamisi, anakiri kwamba kinamama katika mkoa huo wanahitaji elimu kwani bado hawana ufahamu sahihi wa unonyeshaji watoto, na kwamba asilimia 30 pekee ndiyo hunyonyesha watoto wao ndani ya saa moja mara baada ya kujifungua kwa wale wanaojifungulia hospitalini.

Anasema maziwa ya mama kwa mtoto ni muhimu kujenga mustakabali wa afya yake ikiwamo ukuaji kimwili, kiakili, na hata kupunguza tatizo la udumavu ambalo huathiri mwili akili na maisha ya watu.

"Mtoto akizaliwa baada ya saa moja, anapaswa kunyonyeshwa yale maziwa ya kwanza ya njano na siyo kuyakamua na kuyamwaga. Ni kwa sababu yana virutubisho na ni kinga ya mwili ya mtoto na hayana madhara," anasema Hamisi.

Kadhalika anaeleza kuwa wanawake wengi wasio na ufahamu hawapendi kuwanyonyesha watoto wao maziwa hayo ya njano wakidhani ni machafu na kuwanyima watoto kinga ya asili.

Anasema mtoto akishazaliwa licha ya kunyonya maziwa hayo ya njano pia anapaswa kutolishwa chochote mbali na maziwa ya mama ndani ya miezi sita bila ya kupewa kitu chochote wala maji, ushauri ambao umekuwa ukipuuzwa na wanawake wengi na hata kuwasababishia maradhi mbalimbali.

"Mtoto akishafikisha miezi sita ndipo anapaswa kuanza kupewa vyakula vya ziada kwa kuzingatia lishe bora kwa kufuata makundi matano ya chakula, huku pia akiendelea kunyonyeshwa maziwa ya mama hadi akifikishe miaka miwili hapo lazima awe na afya njema,"anafanua Hamis.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Christina Mndeme, anawashauri wanawake popote nchini kuhudhuria kliniki na kujifungulia katika vituo vya huduma za kiafya ili kwanza kujiepusha na hatari zinazoweza kuwapata na watoto wao pia, lakini pia kujifunza elimu ya afya ya uzazi salama, lishe na unyonyeshaji sahihi watoto.

Anasema, tatizo la udumavu kuendelea ni ukosefu wa elimu kwa wazazi, na kutoa maagizo kwa maofisa lishe na wataalamu wa afya, wafanye mikutano ya mara kwa mara na kuelimisha unyonyeshaji na lishe bora hasa maeneo ya vijijini.

"Naelekeza maofisa lishe wote mkoani hapa wasikae ofisini bali waende kutoa elimu ya lishe na uyonyeshaji kwa wananchi, sababu bila kuwapa mafunzo tatizo hili la udumavu kwa watoto linalotokana na kutonyonyeshwa ipasavyo litaendelea kuwepo hapa Shinyanga," anaonya Christina.

Mkuu wa mkoa anatoa maagizo pia kuwa fedha za lishe ziendelee kutolewa kulingana na mpango kazi uliopo ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zake pamoja na kufanya maadhimisho ya siku ya afya na lishe kila robo mwaka kwa mujibu wa muongozo uliopo ili kufikisha elimu ya unyonyeshaji kwa jamii.

Kadhalika, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Dk.Yudas Ndungile, anasema tatizo la udumavu kwa watoto wadogo walio chini ya umri wa miaka mitano mkoani hapo limepungua kutoka asilimia 32.1 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 27.5 mwaka jana.

Anaeleza kuwa udumavu huo umepungua kutokana na elimu ya unyonyeshaji na lishe bora ambayo imekuwa ikitolewa kwa wazazi kupitia huduma za kiafya, na kueleza kwamba bado elimu zaidi ina hitajika kutolewa hasa maeneo ya vijijini.

Mwanamama Careen Jamson, anasema alishapata elimu ya unyonyeshaji katika kituo cha afya Kambarage Manispaa ya Shinyanga, na mtoto wake ambaye kwa sasa ametimiza miezi sita, hakuwahi kumpatia kitu chochote zaidi ya maziwa yake.

Anasema awali hakuwa na elimu hiyo ya unyonyeshaji, lakini sasa hivi elimu anayo na mtoto wake ana afya njema na anaamini hilo limesaidia kumwepusha na maradhi ya mara kwa mara sababu ana kinga ya maziwa ya mama.

Khadija Shabani, anasema baadhi ya wanawake hawataki kunyonyesha watoto wao kwa madai ya kulinda muonekano wa matiti yao wakiamini eti yatapoteza muonekano mzuri.

Anasema elimu bado inahitajika kwa jamii kuhusu faida ya unyonyeshaji watoto ili kuondoa udumavu kwa watoto wao.

## Mabinti wanaorejea darasani baada ya uzazi wana haya...

**INATOKA UK.11**

ya kuimarisha kamati za ushauri na kuzungumza na wanafunzi wenyewe na kuwapa ushauri mara kwa mara ambapo kila wiki shule saba zinafikiwa.

Norbert Nombo mkufunzi mkazi wa mkoa wa Pwani, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, anasema vipo vituo nane ambavyo wanafunzi waliokatisha masomo kwa kupata ujauzito wanahudumiwa.

Anasema kwa kipindi cha miaka miwili wanafunzi 163 ambao wamerudi shule wamerejea katika mifumo miwili tofauti ambayo ni pamoja na ule ulio rasmi wa shule za sekondari ambazo zinasimamiwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) .

Na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imepewa jukumu la kufanikisha elimu nje ya mfumo rasmi na wamepewa kazi ya kuwarudisha mabinti shule na vituo vilivyopokea wanafunzi hao ni pamoja na Mkuranga, Rufiji, Mafia, Chalinze, Mlandizi na Tumbi.

Nombo anaeleza kwamba taasisi hiyo pia inashirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Jupita, Vijaliwa Vingi, Watoto Wetu na Mwinyi ili kusaidia baadhi ya wasichana ambao hawakuwa na walezi wa watoto wao ili waendelee na masomo.

Kwa mujibu wa mkufunzi huyo mradi wa Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari. SEQUIP unalipia ada na vitabu pekee, kwa maana ya kuwalipa walimu wanaofundisha na vifaa vya steshenari na kwamba vituo vya Lukenge na Tumbi Sekondari ni kati ya vinavyopokea wanafunzi hao ambao wanaanza masomo saa nane mchana hadi saa 12 jioni.

Na katika kituo cha Vijaliwa Vingi na Watoto Wetu vinavyochukua wanafunzi hao pamoja na watoto wao, na muda wa mosomo ukiisha wasichana hao wanapata muda wa kukaa na watoto.

Katika mradi huo ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia umewezesha pia ujenzi wa kituo cha kusomea ambacho kimejengwa Kibaha, vyumba vya madarasa vinne, matundu sita ya vyoo na chumba cha kulea watoto.

Nombo anaeleza kwamba tayari kituo hicho kimeshakamilika na wanachosubiri ni samani hasa meza za kusomea ili wanafunzi wahamie.

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN,
ZANZIBAR

# Yasiyowezakana visiwani yanapoanza kushuhudiwa



Wanafunzi wa shule mbalimbali za serikali wakishiriki Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika mwaka huu Mjini Zanzibar. **PICHA :RAHMA SULEIMAN**

NI miaka mitatu sasa tangu kuanzishwa kwa Mahakama Maalumu ya Udhalilishaji Zanzibar ambapo serikali ilichukua hatua hiyo baada ya kushamiri vitendo vya unyanyasaji na kutoridhishwa na namna kesi zake zilivyoshughulikiwa.

Uamuzi huo wa serikali ulipata baraka na kuungwa mkono na wadau wa maendeleo pamoja na wanaharakati wa kutetea haki za wanawake na watoto huku wakiwa na imani kwamba ujio wake ni mwarobaini na ndiko kuvifanya vitendo hivyo historia.

Udhalilishaji wanawake na watoto ni tatizo la ukiukwaji wa haki za binadamu, licha ya juhudi zinazoendelea kuchukuliwa kupiga vita tatizo hilo, lakini limekuwa likiendelea Zanzibar na kuathiri maendeleo ya kundi hilo.

Kwa mujibu wa Mahakama Kuu Zanzibar, tangu kuazishwa kwa mahakama hiyo mwaka 2021/2022 kesi 122 zimeripotiwa'

za kubaka ni 72, za kulawiti 20 wakati ni mashauri 27 pekee yaliyotolewa hukumu na 25 yanaendelea kusikilizwa na kesi zilizofutwa ni 70 kwa sababu mbalimbali ikiwamo kukosekana ushahidi.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kesi zilizofunguliwa katika mahakama maalum ni 432, ubakaji unaongoza kwa kuwa na kesi 191, kulawiti ni 52 hizi ni kesi zinazowahusu watoto wa kiume wakati za kuingiliwa kinyume na maumbile ambazo zinawahusu wasichana ni 60, takwimu za Mahakama Kuu zinabainisha.

Mahakama Kuu inasema kati ya hizo kesi 160 zimefutwa, aidha 74 zimetolewa hukumu na kesi 198 zinaendelea kusikilizwa mahakamani hapo.

"Ilikuwa ni nadra kusikia mshtakiwa wa kesi za udhalilishaji kufungwa miaka 30 au kifungo cha maisha Zanzibar lakini hivi sasa tangu kuazishwa chombo hicho wafungwa wapo. Washtakiwa wanahukumiwa kifungo cha miaka 30 na wengine cha maisha" anasema Fatma Juma.

Fatuma mwanaharakati wa kutetea haki za wanawake na watoto, anaeleza kuwa tangu Serikali ya Zanzibar kuanzisha Mahakama Maalum ya Udhalilishaji, hukumu zinazotolewa kwa baadhi ya kesi hizo zinaridhisha ikilinganishwa na kipindi cha nyuma kabla ya kuwepo kwake.

Anasema imefanikisha kusikilizwa kwa haraka kwa kesi za udhalilishaji na hukumu za vifungo kuongezeka tofauti na hapo awali.

**POLISI WAWAJIBIKA**

Kuazishwa kwa mahakama hiyo kumechangia kasi ya utendaji kazi wa kushughulikia kesi hizo kwa askari na Jeshi la Polisi, anasema kamishna msaidizi wa polisi na mkuu wa madawati ya jinsia, Egyne Emmanuel.

Anasema kulikuwa na msongamano mkubwa wa kesi katika vituo vya polisi, lakini hivi sasa zinapewa kipaumbele na kuongeza uharaka wa kushughulikia makosa hayo.

Katika kuboresha kazi za dawati la jinsia kwenye vituo vya polisi, kupambana na vitendo hivyo, anasema kuna baadhi ya vitendo haviripotiwi polisi kwa sababu ya waathirika kutishwa kutokana na wadhalilishaji kuwa watu wa karibu na familia.

Kamishna Emmanuel anasema, Jeshi la Polisi limeanzisha utaratibu maalumu wa kuwapeleka polisi shuleni kutoa elimu ya usalama kwanza ili kuibua vitendo vya udhalilishaji ambavyo vimefichwa.

Anasema katika mwaka 2022 jeshi hilo limeibua kesi 57 za udhalilishaji shuleni ambazo hazikuripotiwa polisi na mchakato wa kisheria unaendelea.

"Huu ni mwanzo tu tunaamini mpango huu utasaidia kuibua kesi nyingi ambazo haziripotiwi polisi lakini mkakati mwingine ni kutoa elimu kwa jamii kwa sababu makosa mengi ya udhalilishaji ni kwa watoto kuanzia miaka 14 hadi 18,"anasema Emmanuel.

Anaongeza kuwa elimu hiyo itasaidia kuongeza kiwango cha uelewa ili jamii ielewe ni umri gani wa kushiriki tendo la ndoa badala ya kuwepo kwa kesi nyingi za watoto kujihusisha na kujamiiana wakiwa na umri mdogo.

Aidha, anasema mkakati mwingine ni kuongeza idadi ya madawati kwa sababu yaliyopo ni machache na hayapo katika kiwango bora na kwa sasa kuna idadi ya madawati matatu ambayo yamefikia kiwango cha kuwa dawati hivyo wanahitaji kuwa na madawati 57 yenye viwango.

"Ili dawati liwe na kiwango kwanza linatakiwa kuwa nje ya kituo cha polisi kuwe na vyumba maalum kwa ajili ya kumhoji mtoto, viwepo na vitendea kazi ikiwamo usafiri," anasema

Aidha, mkakati mwingine ni kuboresha ukusanyaji wa taarifa kwa sababu utaratibu wanaotumia hivi sasa umepitwa na wakati, wawe na vifaa vya kieletroniki badala ya kusubiri kesi itokea wilayani hadi makao makuu.

"Mpango mwingine ni kuboresha usafiri kwa watendaji wetu hasa kuwa na pikipiki kwa watendaji wa dawati ili kuharakisha ufuatiliaji wa kesi ikiwemo kufanya uchunguzi wa haraka,"anasema.

> Ili dawati liwe na kiwango kwanza linatakiwa kuwa nje ya kituo cha polisi kuwe na vyumba maalum kwa ajili ya kumhoji mtoto, viwepo na vitendea kazi ikiwamo usafiri.

**KUCHUNGUZA DNA**

Amina Said Abdallah, mchunguzi wa maabara katika Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar, anasema kwa mwaka 2021/2022 wamepokea kesi 95 za udhalilishaji kwa ajili ya kuchunguza vinasaba (DNA).

Halikadhalika, kesi nyingi zinazofikishwa hapo baada ya kufanyiwa uchunguzi mhusika anatambulika na asilimia 80 ya washukiwa hupatikana wakati asilimia 20 ya washukiwa wanabainika kubambikizwa kesi, anasema.

Ushahidi wa vinasaba unapokuwa mahiri kazi ya uchunguzi huwa nzuri na huchukuwa muda wa wiki mbili kukamilika, anaongeza.

Aidha, anaitaka jamii kutowasafisha watoto waliofanyiwa vitendo vya udhalilishaji ili kuzuia kupoteza ushahidi na watuhumiwa kutotiwa hatiani.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) inasema utendaji wa mahama ya udhalilishaji ni mahiri na umesaidia katika uendeshaji wa kesi hizo kwa haraka.

Huda Khamis wakili wa serikali kutoka ofisi ya DPP, anasema jalada la kesi za udhalilishaji linapofika katika ofisi ya Mkurungenzi wa Mashtaka halichukui muda mrefu kama ushahidi utajitosheleza na si zaidi ya wiki mbili kesi hushughulikiwa na kufikishwa mahakamani.

Huda anasema licha ya uwepo wa mafanikio baada ya kuanzishwa kwa mahakama hizo lakini bado jamii inamuhali na baadhi yao hukataa kufika mahakamani kutoa ushaidi.

"Bila ya ushahidi hakuna hatia wakati mwingine tunalaumu kuwa washitakiwa wanaachiwa huru lakini kwa upande mwingine kesi zinakosa ushahidi jamii bado ina muhali au kuoneana aibu kwa sababu wafanyanyaji wa vitendo hivyo ni watu wa karibu katika familia za wahanga,"anasema.

**SAUTI ZA WAHANGA**

Wahanga wa vitendo vya udhalilishaji wanasema bado hawaridhiki na uendeshwaji wa kesi wa mahakama ya udhalilishaji na miongoni mwa sababu wanazozitaja, ni kuchukuwa muda mrefu kutoa hukumu.

Amina Juma (sio jina halisi) mzazi wa mtoto aliyebakwa anasema washitakiwa wanadanganya mahakamani kwa kudai wana umri mdogo kuzuia haki kutendeka.

"Mtoto wangu wa miaka 12 alifanyiwa kitendo cha udhalilishaji lakini nashangaa baada ya mtuhumiwa kufikishwa mahakamani alidanganya umri kuwa ana miaka 16 wakati taarifa zake za mwanzo za kituo cha polisi zinaeleza ana miaka 19,"anasema.

ELIMU

NA DK FELICIAN B. KILAHAMA

# Ni wakati wa kutafakari vijana watakavyotumika kunufaisha taifa

TAKWIMU za mwaka huu 2023 za Shirika la Idadi ya Watu (UNFPA), zinaeleza kuwa dunia inakaliwa na watu bilioni 7.954, Afrika pia haipo nyuma kwa maana idadi ya watu wake inafikia bilioni 1.372.

Watanzania ni takribani milioni 62 kwa mujibu wa ripoti ya sensa ya watu na makazi ikiwa ni sawa na asilimia 4.5 ya idadi ya watu barani Afrika.

Kimsingi hiyo ni nguvukazi muhimu ya kujiletea maendeleo endelevu iwapo itajengewa uwezo na ikatumika kwa umakini na nidhamu.

Katika ripoti hiyo ya sensa ya 2022, nguvukazi nchini imegawanywa katika makundi mawili. vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 35 ikiwa ni takribani milioni 21 sawa na asilimia 34.5 ya Watanzania wote na kundi la pili ni la wenye umri kati ya miaka 15 na 64.

Hawa ni watu wazima pamoja na umri zaidi ya miaka 60 mpaka 64 wakiwa ni sehemu ya wazee lakini bado wana nguvu ya kufanya kazi. Hivyo idadi yao ni takribani milioni 32 sawa na asilimia 53.4 ya Watanzania wote.

Nimekisia kuwa nguvukazi vijana ni kati ya miaka 15 na chini ya miaka 45 idadi yao ikiwa kama watu milioni 26. Waliobaki, umri chini ya miaka 15 na umri wa zaidi ya miaka 45 ni makundi ya watoto na watu wazima, wazee na vikongwe.

Kwa mantiki hiyo idadi ya vijana katika uhalisia wao, na kama nguvukazi muhimu ya taifa ni wengi na swali ni hili, nini hatima yao katika kuyatimiza malengo ya taifa ya kujiletea maendeleo endelevu?

Iwapo watu zaidi ya milioni 26 watajengewa uwezo wa kasimamiwa ipasavyo na kutumika vizuri na kwa nidhamu kubwa, hakuna shaka taifa litajiletea maendeleo endelevu kupitia sekta mbalimbali ikiwamo kilimo, ufugaji, misitu na nyuki, uvuvi na shughuli kadhaa za utalii, biashara na ujasiriamali.

Kikubwa cha kukisimamia ni hiki kama taifa linaloendelea je, tunatumiaje vijana waliopo ili kuyafanikisha malengo hayo?

Tunaposema nguvukazi ni muunganiko wa maneno mawili nguvu ambao ni uwezo wa kufanya jambo au kitu fulani au kuwa na madaraka kisiasa na kiutawala. Kwa neno kazi linamaanisha utumiaji wa nguvu au nishati ama juhudi, maarifa katika kufanikisha kitu au jambo fulani.

Kwa msingi wa maelezo hayo, taifa linalo uwezo wa kufanya au kutekeleza shughuli zake bila vikwazo vingi kwa mantiki kwamba wapo wa kutosha kuendesha mambo yake kwa lengo la kujitegemea zaidi na kujiletea maendeleo endelevu.



Vijana wengi wanaendesha pikipiki, nguvu yao inahitajika zaidi kuinua uchumi kwa kufanyakazi zenye tija. **PICHA: MTANDAO**

> “Pamoja na ukweli kwamba, kwa miaka mingi tulikosea, serikali iliyopo madarakani inastahili pongezi kwa kuziona changamoto za nguvukazi ya vijana.

Ndiyo maana baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere aliweka bayana kuwa ili taifa lijiletee maendeleo linahitaji vitu vya msingi vinne, watu wa kutosha wenye nguvu za kufanya kazi, ardhi, siasa safi na uongozi bora

Suala la vijana nguvukazi ya taifa linahitaji kufanyiwa mikakati ili nchi inufaike nayo na kwanza kuelewa kuwa Tanzania ni taifa linaloinukia kiuchumi na shughuli zake nyingi bado zimeegemea kwenye kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na nyuki na biashara kama usafirishaji na mawasiliano (TEHAMA),

Aidha, kwenye uhifadhi, uendelezaji na usimamizi au utumiaji endelevu wa maliasili zetu na utalii. Maeneo hayo yote yanahusu kufanya kazi kwa kutumia watu ambao ni vijana wengi tulio nao hapa nchini.

Pili, tunahitaji mikakati shirikishi ya kitaifa ili kuhakikisha vijana hao wanaume kwa wanawake, wanatumika ipasavyo, bila ya kutegemea sana misaada kutoka mataifa mengine.

Miaka iliyopita serikali iliweka mkazo kwenye masuala ya kilimo. Tulikuwa na kaulimbiu zilizolenga kuhamasisha na kuboresha shughuli za kilimo. Mathalani, ‘siasa ni kilimo, kilimo cha kufa na kupona, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi’.

Pamoja na hayo yote, kiuhalisia utekelezaji haukuendana na mitazamo hiyo. Hivyo, masuala ya kilimo hayakupewa kipaumbele na msukumo halisi kama ilivyotarajiwa.

Kwa mfano, shughuli za ugani zikawa zinasuasua na upatikanaji wa vifaa kazi kama matrekta au majembe ya kukokotwa na wanyama na pembejeo zikiwamo mbegu bora, viwatilifu, huduma za kusindika mazao na masoko, ikawa changamoto zaidi.

Hali kama hiyo iliwakumba pia wavuvi, wafugaji na wakulima wa mazao ya misitu/ufugaji nyuki.

Pamoja na ukweli kwamba, kwa miaka mingi tulikosea, serikali iliyopo madarakani inastahili pongezi kwa kuziona changamoto za nguvukazi ya vijana.

Aidha, imeongeza bajeti ya kilimo kwa nia njema ya kuziwezesha shughuli za kilimo kuwa zenye manufaa makubwa kwa Watanzania na zaidi vijana wenye utayari wa kutaka kujiendeleza kiuchumi na kwa manufaa ya taifa.

Iwapo umuhimu wa kilimo, ufugaji na uvuvi katika kufanikisha lengo la kujiletea maendeleo endelevu utazingatiwa na fedha zilizotengwa takribani trilioni moja katika mwaka wa fedha 2023/2024 na kuelekezwa kwenye sekta ya kilimo; zitapatikana kwa wakati muafaka na kusimamiwa tena kutumika kwa malengo yaliyowekwa na kwa umakini mkubwa hatimaye kuwasaidia vijana wengi kumudu changamoto za kimaisha litakuwa jambo jema.

Pamoja na kuongeza bajeti kubwa ni kuhakikisha kuwepo na mikakati mahususi ili kiasi kilichotengwa kitumike kuboresha uzalishaji wa mali na mazao kupitia rasilimali ardhi hususani huko wilayani na vijijini kwa kutumia sehemu ndogo ya ardhi na kupata mazao mengi kwa ekari au hekta moja.

Iwapo kutatokea changamoto, jitihada zifanyike haraka kuzitafutia ufumbuzi kupitia wataalam na washauri na vyombo vingine kama vyama vya ushirika na serikali za mitaa katika halmashauri zinazohusika.

Kwa sasa changamoto kubwa kwa vijana ni wengi kutoka vijijini na kuhamia mijini na kwenye majiji kama Dar-es-Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya. Hali hii huhamisha nguvu kazi hiyo kutoka vijijini kwa lengo la ‘kutafuta maisha’ bora zaidi kwenye miji, manispaa na majiji.

Hali hiyo, inaonyesha kuwa kuna mtazamo kwamba kwenye miji na majiji kuna uwezekano wa kupata fedha za harakaharaka bila kujali mazingira watakayokumbana nayo.

Mtazamo kama huo siyo dalili njema kwa mustakabali wa taifa na watu wake kujiletea maendeleo.

Kwa miaka miwili iliyopita kasi ya vijana kujipatia fedha za haraka au chapuchapu imeongezeka sana na sasa sehemu kubwa wamejiingiza kwenye michezo ya kupata fedha kupitia kubet, wakibashiri timu za mipira zitakazo shinda mechi mbalimbali kwa kuziwekea matokeo.

Mathalani, kubashiri timu gani itashinda, idadi ya magoli, muda yatakayofungwa na wafungaji kadhalika ipo michezo mingine mingi kupitia mitandao na vyombo mbalimbali vinavyohimiza Watanzania kucheza ili kujipatia fedha kirahisi.

Haya yote yanafanyika kwa misingi ya kamari na vijana wengi wamevutwa na hali hiyo mambo hayo yanayoongeza tafakauri na kuandaa mbinu bora za kusaidia nguvu kazi hiyo iwe na tija kwa taifa.





# Wagonjwa 10,000 wafanyiwa upasuaji mabusha, matende

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAGONJWA 10,000 wamefanyiwa upasuaji wa mabusha na matende kupitia kambi za madaktari zilizowekwa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, Dk. George Kabona aliyasema hayo jana alipokuwa akifafanua juu ya magonjwa matano makubwa ambayo ni matende, mabusha, kichocho, minyoo ya tumbo na vikope.

Alisema katika kambi hizo walitambuliwa wagonjwa zaidi ya 22,000 na kati yao 10,000 walifanyiwa upasuaji.

Dk. Kabona alibainisha pamoja na kufanya upasuaji pia waligawa dawa kwa kaya mbalimbali ili kuhakikisha kila mtu mwenye magonjwa hayo anapata tiba stahiki ili kuondokana na tatizo hilo.

Alisema serikali imeweka mkakati wa kuwatambua wagonjwa wa aina hiyo ili kuhakikisha inaimarisha mifumo ya utoaji tiba ili kuhakikisha wanazuia dalili za magonjwa hayo, ikiwamo kuyatokomeza kabisa.

Alieleza kuwa moja ya mkakati ambao serikali imeweka ni kuhakikisha wanatoa tiba kwa wagonjwa lakini pia wanagawa dawa katika kaya na shuleni ili kuzuia magonjwa hayo kama sio kuyatokomeza kabisa.

Akizungumzia ugonjwa wa vikope, alisema halmashauri 69 ziliathirika kutokana na utafiti uliofanyika mwaka 2004 hadi 2012 na tayari serikali ilishagawa dawa kwa sasa zimebaki halmashauri 9 zenye ugonjwa huo.

Alifafanua kuwa sababu kubwa ya ugonjwa huo kuendelea kuwepo kwenye halmashauri hizo 9 ni ukanda wa wafugaji.

Naye, Mwenyekiti wa kupambana na malaria na magonjwa yasioambukiza, Riziki Lulida, alisema taasisi yao ilianzishwa kwa lengo la kupambana na magonjwa hayo ili kuhakikisha malaria na magonjwa mengine yanatokomezwa kwa kiasi kikubwa.



Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali linalotoa elimu kuhusu masuala ya huduma za kijamii la Himiza Development Organization (HDO) la Mkuranga mkoani Pwani, Prisca Ngweshemi, akitoa taarifa ya utendaji wa shirika hilo kwa wadau wa maendeleo ya jamii waliotembelea shirika hilo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Kamati ya Bunge yaipa 5 h'shauri ujenzi vitega uchumi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ameipongeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kuwekeza vitega uchumi mbalimbali vya kudumu vyenye lengo la kuimarisha mapato.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Stanslaus Mabula, alitoa kauli hiyo jana kwenye ziara ya kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa kupitia fedha za boost, mapato ya ndani na fedha kutoka serikali kuu.

Alisema majiji mengi hayana miradi kama hiyo ya Dodoma na linaonesha kukua kwa kasi.

"Miradi kama hii inahitaji wawekezaji wazuri ili iendelee kuwanufaisha kwahiyo inatakiwa mfanye jitihada ili ifanye kazi vizuri hongereni na msichoke kuendelea kuwekeza na kuwaza miradi mikubwa zaidi," alisema.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alisema uwapo wa ukumbi wa mikutano na hoteli ya Jiji unawarahisishia ufanisi wa kazi wageni wanaofika mkoani humo.

Kamati hiyo ilikagua ujenzi wa wodi za watoto, wanawake na wanaume katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, ujenzi wa Shule ya Msingi Moleti inayojengwa kupitia fedha za mradi wa boost.

**Alisema majiji mengi hayana miradi kama hiyo ya Dodoma na linaonesha kukua kwa kasi.**

# Dk. Jingu: Uboreshaji familia utapunguza watoto mitaani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JAMII imetakiwa kuimarisha familia ili kuondokana na wimbi la watoto waishio na kufanya kazi katika mazingira magumu.

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. John Jingu, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wadau mbalimbali wanaohusika na usimamizi na utekelezaji wa afya ya ulinzi na usalama wa mtoto nchini jijini hapa.

Alisema katika kuhakikisha taifa linaondokana na tatizo la mmomonyoko wa maadili ni muhimu kuimarisha familia kwenye malezi.

"Wazee wa kimila na watu wa dini ni vyema kuwapa vijana elimu ya maisha ya ndoa kabla hawajaingia huko kwani changamoto nyingi huibuka baada ya familia kuvunjika na waathirika wakubwa huishia kuwa watoto na mwisho wa siku kujikuta katika mazingira yasiyo rafiki kwa makuzi yao,"alisema.

Naye, Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii Baraka Makona, alisema serikali inaendelea kukabiliana na tatizo hilo kwa kuwakusanya na kuwalea katika makao ya kulelea watoto Kurasini na Kikombo.

Mwakilishi wa Shirika la PACT Tanzania, Flora Kitato alipongeza serikali kwa jitihada zake za kupambana na wimbi hilo na kuahidi kuendelea kufanya kazi bega kwa bega na serikali ili kuhakikisha watoto wanaishi katika mazingira salama na yenye ulinzi.

# Vijana wapewa mbinu za kujikwamua kiuchumi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA wametakiwa kutumia fursa zilizopo kujikwamua kiuchumi na kuacha kuiga mila na desturi za mataifa mengine ambazo haziendani na tamaduni zao.

Mwenyekiti wa Bunge, David Kihenzile, aliyasema hayo juzi kwenye Kongamano la Vijana na Demokrasia lililofanyika jijini hapa. Alisema vijana wanapaswa kuchangamkia fursa mbalimbali ambazo zimekuwa zikitolewa na serikali na kuacha kulalamika vijiweni.

Alibainisha Tanzania ina rasilimali nyingi ambazo kama zitatumiwa vizuri na vijana zinaweza kuwakwamua kiuchumi na kupunguza malalamiko ya uhaba wa ajira nchini.

"Tanzania ina madini mengi, mifugo mingi lakini pia ardhi kubwa ambayo inafaa kwa kilimo hivyo vijana kama watatumia vizuri rasilimali hizi wataweza kujikwamua kiuchumi na kujiongezea kipato,"alisema.

Vilevile, alisema ipo haja kwa taifa kuanza kuandaa vijana ambao watakuja kuliongoza taifa katika misingi ya uadilifu na uzalendo.

"Lazima kama taifa tuwe na watu ambao watakuja kuliongoza taifa hili ambao wataweza kulinda rasilimali zetu hivyo lazima kuwa na vijana ambao wana elimu ya kutosha, waadilifu, wazalendo na wanaolijua taifa lao ipasavyo,"alisema Kihenzile.

Pia, alisema ipo haja kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kuwa inaharakisha mchakato wa kupatikana kwa Baraza la Vijana ili kundi hilo kubwa nchini kuwa na eneo rasmi la kuzungumzia mambo yao.

"Mimi niwahakikishe kuwa nitazibeba hoja zote za vijana na kuzifikisha kwenye vikao vya maamuzi kama ambavyo mkuu wa nchi Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha nia kubwa ya kujali kundi hili ambalo linaongoza kwa kuwa na watu wengi nchini kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi."

"Ushauri wangu kwa vijana ametuambia hapa mkurugenzi wa vijana kuwa kama taifa tuna mifuko ya vijana ya mikopo lakini wangapi wanafahamu?,wengi wanafahamu kuwa asilimia 10 ya manunuzi ya serikali inapaswa kwenda kwa kundi la vijana? hakuna anayefahamu, hivyo fursa hizi ni lazima tuzipambanie tusisubiri kuletewa,"alisema.

Naye, Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Dk. Michael Battle, alisema vijana wa kitanzania ndiyo wenye nafasi ya kuamua taifa hilo liwe la namna gani hapo baadaye kutokana na nguvu kazi iliyopo kwa kundi hilo nchini.

"Vijana mnapaswa kutambua kuwa nyinyi ndiyo wenye jukumu la kulitengeneza taifa hili liwe na namna gani, hivyo mnapaswa kuwa sehemu kubwa ya kulijenga taifa hili ili liwe imara au vinginevyo,"alisema.

Kadhalika, alisema vijana wanapaswa kufanya mambo yao kwa mujibu mila na desturi za taifa lao na kuacha tabia ya kuingia tamaduni za mataifa mengine.





# Wakulima kuiburuza kortini kampuni Mkwawa kisa malipo

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKULIMA wa tumbaku wa Chama cha Msingi cha Mtande (Mtande AMCOS) cha wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, wametishia kuvunja mkataba na kuiburuza mahakamani kampuni ya ununuzi wa zao hilo ya Mkwawa endapo haitawalipa fedha zao.

Hivyo, wametoa siku tano kwa kampuni hiyo kuwalipa fedha zao ili waendelee na shughuli zao, huku wakisisitiza kuwa wasipolipwa katika kipindi hicho watachukua hatua.

Waliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano maalumu na kueleza kuwa wamechoshwa na ahadi za mara kwa mara ambazo kampuni hiyo imekuwa ikiwaahidi mara kwa mara bila kutekeleza jambo ambalo linawakwamisha kuanza maandalizi ya msimu ujao wa kilimo.

Mmoja wa wakulima hao, Zawadi Chance, alisema kampuni hiyo ilichukua tumbaku yao tangu Juni na iliwaahidi kwamba ingewalipa ndani ya muda mfupi lakini mpaka sasa haijawalipa hali ambayo imezua wasiwasi miongoni mwao.

Alisema kuchelewesha kwa malipo hayo kumesababisha migogoro mingi ikiwemo ya kifamilia pamoja na migogoro kati ya wakulima na wafanyakazi ambao waliwaajiri kushirikiliana nao kwenye uzalishaji.

"Sasa hivi hata kwenye familia hatuelewani kwa sababu ya hawa watu, tunazalisha tumbaku ili fedha tunazopata zitusaidie kuendesha maisha ya familia zetu, lakini pia kuna vibarua ambao tumesaidiana nao kwenye uzalishaji wanatakiwa kulipwa, hatuwezi kuwalipa kwa sababu na sisi hatujalipwa lakini hawatuelewi," alisema Zawadi.

Mkulima mwingine, Nelson Underson, alisema kitendo cha kampuni hiyo kuchelewesha malipo kinawasababisha kushindwa kuwaamini viongozi wao wa vyama vya msingi wakiamini kuwa kuna uwezekano wanakula njama na kampuni hiyo.

Aliwaomba viongozi wa AMCOS kuwasiliana na kampuni hiyo ili kujua hatima ya malipo yao akisisitiza kuwa kwa sasa wanatakiwa kuanza maandalizi ya msimu mpya wa kilimo, hivyo ni vema wakalipwa mapema fedha zao.

Mwenyekiti wa AMCOS hiyo, Richard Mbalamwezi, alisema tayari wamechukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kuonana na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kumueleza kuhusu tatizo hilo.

Alisema Waziri Bashe aliwaambia kuwa alishapata taarifa zao lakini tatizo lililopo ni uhaba wa dola na hivyo akawataka wananchi kuendelea kuwa wavumilivu wakati tatizo lao linashughulikiwa.

"Sisi kama viongozi wenu hatujakaa kimya, tumekuwa tukifuatilia kuhusu fedha zetu maana hata sisi ni wenzenu na tunaumia pia, tumeshatoa taarifa kwa viongozi wetu wa wilaya na hata Waziri wa Kilimo," alisema Mbalamwezi.

Akizungumza kwenye mkutano wa wanachama wa Mtande AMCOS, Meneja wa Kampuni ya Mkwawa, Godluck Mnasa, alikiri kuwepo kwa tatizo hilo la kuchelewesha malipo na kwamba tatizo lililopo ni uhaba wa dola.

Alisema tatizo hilo kwa sasa limeshapatiwa ufumbuzi na kwamba kampuni hiyo itawalipa fedha zao kabla ya Agosti 24 mwaka huu na kwamba watahakikisha kila mkulima analipwa fedha zake.



Mmoja wa wanachama wa Chama cha Wakulima wa Tumbaku wa Mtande AMCOS, wilayani Chunya, mkoani Mbeya, Nasika Alan akizungumza kwenye mkutano wa chama hicho mwishoni mwa wiki, uliolenga kujadili ucheleweshaji wa malipo ya mazao yao unaofanywa na kampuni ya ununuzi wa tumbaku ya Mkwawa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Agizo la Samia latokomeza vitendo ubakaji, unyang'anyi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI mkoani Njombe wamesema utekelezaji wa ahadi ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika ufungwaji wa taa barabarani katika wilaya tatu utasaidia kuondokana na vitendo viovu ukiwemo ubakaji na unyang'anyi.

Wakizungumza na Nipashe walisema wanaishukuru serikali kwa kutimiza ahadi hiyo na kwamba hapo awali walikuwa wanapata tabu kwa sababu ya kukosa mwanga wakati wakifanya shughuli zao majira ya usiku.

"Hizi taa zinatusaidia kila sehemu wakati kuna giza tuliibiwa sana, wanawake walikuwa wanafanyiwa ubakaji lakini hivi sasa unamuona anaekuja mbele yako tofauti na mara ya kwanza" alisema Daniel Kihombo ambaye ni mfanyabiashara.

Naye Martin Luvanda mkazi wa Lwawa wilayani Makete aliwataka wakazi wa maeneo ambayo zimefungwa taa za barabarani kuitunza miundombinu hiyo kwa sababu imejengwa kwa gharama.

Alisema: "Hapa tumeona zimewekwa taa basi tuweke ulinzi wa miundombinu iliyowekwa ili taa tuendelee kuziona lakini pia tuiombe serikali taa zimewekwa lakini sio eneo kubwa sana tunategemea kuona mji wetu unakuwa taa nyingi zaidi"alisema Luvanda.

Meneja wa TANRODS Mkoa wa Njombe, Mhandisi Lucy Shalua, alisema zaidi ya taa 70 zimefungwa katika wilaya tatu za Makete, Njombe na Wanging'ombe.

Alisema: "Bado tunaendelea kufunga katika maeneo mengi, tumeweka utaratibu wa kufanya matengenezo kwa muda wote, sasa hivi kuna mkandarasi amezifunga na ameziwasha ziko kwenye muda wa matazamio kwa hiyo baada ya muda wa matazamio kuisha hata kukitokea changamoto ina maana tutazirekebisha ili ziweze kuhudumia kwa muda wote".

# Madiwani wanunua simu janja zisajili wanachama CCM

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wamenunua simu 26 na kuzikabidhi kwa uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya kusajili wanachama wa chama hicho kwenye kata zote za wilaya hiyo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mpokigwa Mwankuga, alikabidhi simu hizo kwa viongozi wa CCM mwishoni mwa wiki wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa chama hicho ngazi ya kata ambayo yaliandaliwa na Idara ya Uenezi.

Mwankuga alisema, madiwani hao walikubaliana kuchangishana fedha kwa ajili ya kununua simu hizo ili kukisaidia chama kurahisisha kazi ya kusajili wanachama katika ngazi ya kata.

Alisema kati ya simu hizo 25 zilinunuliwa na madiwani wote lakini simu moja ilinunuliwa na madiwani wa viti maalumu kwa ajili ya Jumuiya ya Wanawake wa chama hicho ngazi ya Wilaya.

Alisema ununuzi wa vifaa hivyo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya chama ya kuhakikisha wanakisaidia chama kutekeleza majukumu yake hasa ya kuimarisha chama kwa kusajili wanachama.

"Simu hizi tumezinunua kwa Sh. milioni 4.1, tutaomba mzipokee simu hizi ili zikakisaidie chama kwenye usajili wa wanachama wapya, tunaamini kwamba zikitumike vile inavyokusudiwa basi chama kitaimarika," alisema Mwankuga.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Rungwe, Mekson Mwakipunga, alisema pamoja na simu hizo lakini madiwani hao wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kukisaidia chama kwenye majukumu mengine ya kiutendaji kwa kutoa michango mbalimbali.

Alisema wamekuwa wakitekeleza vizuri utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho kwa kuhakikisha miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao inakuwa na viwango vinavyotakiwa.

Alisema baada ya kupokea simu hizo wanakusudia kuagiza kadi zaidi ya 5,000 kwa ajili ya kuzigawa kwa wanachama watakaokuwa wanasajiliwa kwa maelezo, kwa sasa wanatakiwa kuwapatia wanachama kadi za kielektroniki.

Alisema uhitaji wa kadi hizo kwa sasa ni mkubwa na kwamba simu hizo zimefika muda mzuri ambao ndio zilikuwa zinahitajika zaidi kwa ajili ya kusajili wanachama.

Akipokea simu hizo kwa niaba ya chama hicho, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Ndele Mwaselela, aliwapongeza madiwani hao kwa kuamua kukisaidia chama vifaa hivyo kwa ajili ya kusajili wanachama.

Alisema kitendo walichokifanya madiwani hao ni cha kuigwa na madiwani wa halmashauri zingine za mkoa huo hasa kwenye kukisaidia chama kutekeleza majukumu yake.

Alisema mambo yanayofanyika wilayani Rungwe yanaifanya wilaya hiyo kuwa darasa kwa wilaya zingine za mkoa huo kwa maelezo, mbali na kutolewa kwa simu hizo pia wilaya hiyo ndiyo imekuwa ya kwanza kutoa mafunzo kwa viongozi.

"Hongereni kwa kazi nzuri, hapa mmetoa darasa kwa madiwani wa maeneo mengine, ninyi mmeonyesha kweli mnakipenda chama ambacho kiliwapa nafasi ya kukiwakilisha," alisema Mwaselela.

Aliwataka viongozi wa kata watakaokuwa wanazitumia simu hizo kusajili wanachama wazitumie vizuri ili zitumike kwa muda mrefu na kukisaidia chama kufikia malengo yake.



# Wakulima wa kilimo hai waomba kutengewa masoko

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKULIMA wa kilimo hai wameiomba serikali kutenga masoko maalum kwa ajili yao ili kuwa na soko la uhakika.

Pili Kashinje, mkulima wa kilimo hai wa Kijiji cha Mahonda, Mkoa wa Kaskazini Unguja, aliyasema hayo Mjini Zanzibar wakati wa mkutano wa tathmini wa mradi wa viungo, mboga na matunda unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU).

Alisema litakapotengwa soko maalum la mazao ya kilimo hai jamii watatambua kwa urahisi mazao yatokanayo na kilimo hicho kinapopatikana.

"Masoko yapo mengi sana yamejengwa lakini tunaomba yatengwe masoko ya mazao ya kilimo hai pekee, kuliko kuchanganya mazao ya kilimo hai na mengineyo," alisema.

Alisema hali hiyo inawafanya wakulima wa kilimo hai kukosa soko la uhakika katika kuuza mazao yao.

Aidha, alisema licha ya wakulima kuingia katika mnyororo wa thamani lakini wanakabiliwa na changamoto ya vifungashio vyenye ubora.

"Tunaomba wadau na serikali watusadie sisi wajasiriamali kupata vifungashio vyenye ubora, tunazalisha bidhaa nzuri lakini vifungashio havina ubora"alisema.

Ali Mbarouk, Meneja wa Ufuatiliaji na Tathmini, wa mradi wa viungo, mboga na matunda, alisema katika utekelezaji wa miaka mitatu mradi huo umefikia asilimia 50 ya mafanikio.

Alisema mradi umefanikiwa kutoa huduma ya miundombinu ya maji kwa wakulima kwa sababu kilimo kinahitaji maji, lakini pia mradi umefanikiwa kutoa elimu ya kilimo cha kisasa kwa wakulima.

Kuhusu kuyafikia masoko ya nje katika kilimo cha viungo, alisema bado kuna changamoto katika kuyafikia masoko ya nje ya nchi katika bidhaa za viungo, hivyo mradi unafanya kampeni za kuyafikia masoko ya nje.

**Alisema litakapotengwa soko maalum la mazao ya kilimo hai jamii watatambua kwa urahisi mazao yatokanayo na kilimo hicho kinapopatikana.**

Naye Makame Kitwana Makame, Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Kilimo Zanzibar, alisema katika kuyafikia masoko ya nje kuna haja ya kuzipitia sera za kilimo na wizara ipo katika hatua za mwisho za kufanya mapitio ya sera ya kilimo.

Aidha, alisema wizara pia imendaa mkakati wa mazao ya viungo ambao tayari umeshazinduliwa ambao utasaidia kuyafikia masoko ya nje na ndani.

Makame ambae pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri wa Mradi wa Viungo, alisema kupatikana kwa mazao ya kilimo hai ni moja kati ya utashi wa kila mmoja, hivyo wizara inatarajia kuandaa siku maalum kwa ajili ya kuwa na masoko ya mazao ya kilimo hai.

Alisema lengo kuu ni walaji kutofautisha mazao yaliozalishwa kwa kilimo hai na yasio ya kilimo hai.

Alisema uzalishaji wa mazao ya kilimo hai huwa na gharama kuliko uzalishaji wa mazao ya kawaida, hivyo bei zake huwa ni tofauti ambapo kiafya ni bora zaidi mazao ya kilimo hai kwa sababu huwa hayana kemikali.

## Wanaobeza, kukashifu viongozi wamchefua kigogo CCM

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, amekemea kitendo cha baadhi ya watu ambao wanawabeza viongozi wa kitaifa kwa kuwakashifu.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na viongozi, wanachama wa CCM na wananchi kutoka Chaani, Mkwajuni na Tumbatu Wilaya ya Kaskazini A Unguja, ikiwa ni muendelezo wa ziara yake ya kuimarisha chama.

Alisema wapo baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani ambao wana malengo ya kukichafua CCM na viongozi wake, hivyo ni vyema kwa wana CCM kuwapuuza na kuendelea na uimarishaji wa chama kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Aidha, aliwataka wanachama wa chama hicho kuwa na umoja na mshikamano na kuachana na makundi, majungu na mifarakano ili kutowapa mwanya wapinzani.

Awali, Abdullah ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alikabidhi kwa Mwenyekiti wa Chaani vifaa vya ujenzi ikiwemo matofali 200, saruji mifuko 100, mawe gari mbili, vifusi na mchanga gari moja vilivyotolewa na Mwakilishi wa Chaani, Nadir Abdullatif kwa ajili ya ujenzi wa Tawi la CCM Pwani Mchangani B na ujenzi wa Kituo cha Afya Kandwi.

Naye, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja, Ali Makame Khamis aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kusimamia misingi ya mapinduzi ya Zanzibar pamoja na muungano.

**Alisema wapo baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani ambao wana malengo ya kukichafua CCM na viongozi wake, hivyo ni vyema kwa wana CCM kuwapuuza na kuendelea na uimarishaji wa chama kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.**



Maji machafu yanayotoa harufu mbaya yakiwa yametuama kwenye mitaro ya barabara ya Sewa, Mikocheni Viwandani, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana na kusababisha usumbufu. **PICHA: JULIETH NG'OMA/ TUDARCo**

## Mama Mwinyi ahimiza wanawake kutumia bidhaa za mwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mama Mariam Mwinyi, amewataka wanawake kuongeza matumizi ya bidhaa zinazotokana na mwani.

Amesema zao hilo lina virutubisho vingi, vinaimarisha afya hasa kwa wajawazito.

Mama Mariam ambaye ni Mke wa Rais wa Zanzibar, alisema virutubisho vilivyomo katika zao hilo la mwani ni nadra kupatikana kwenye mazao mengine.

Aliyasema hayo wakati akikabidhi vifaa vya kuanikia mwani kwa wakulima wa mwani Zanzibar kwenye Uwanja wa Bweleo, Wilaya ya Magharibi 'B', Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema mwani huimarisha ustawi wa jamii kwa kupugunza vifo vya mama na watoto vinavyotokea wakati wa uzazi kutokana na wajawazito kupata matatizo ya upungufu wa damu.

Pia, aliitaka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, washirikiane na wadau wengine kuendelea kulitangaza zao la mwani kitaifa hadi kimataifa ili kuliongezea soko kwa ajili ya wakulima wa ndani na kujulikana duniani kote.

Aidha, aliisifu Zanzibar kuwa nchi ya kwanza Afrika kwa ubora wa kilimo cha mwani na uzoefu wa zaidi ya miaka 20 ya kilimo hicho na kuendelea kushika kasi ya uzalishaji duniani.

Hata hivyo, aliwataka wakulima hao kuvitunza vyema vifaa hivyo ili vidumu na kuwasisitiza vijana kuitumia fursa ya kilimo cha mwani kujinufaisha kiuchumi.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Baluu na Uvuvi, Dk. Suleiman Aboud Jumbe, alipongeza taasisi hiyo kwa juhudi ya kuwasaidia kinamama na vijana kwenye nyanja mbalimbali za kiuchumi.

Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Nyabenyi Tipo, aliahidi kuendelea kuwasaidia wakulima wa mwani na kuendelea kuunga mkono harakati za maendeleo kwa serikali zote mbili.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa ZMBF, Fatma Fungo, alisema tayari taasisi hiyo imewaunga mkono kinamama na vijana kutoka vikundi 18 vya wakulima wa mwani kwa Unguja na Pemba ikiwemo kuwapatia vifaa vya kisasa vya ukulima wa zao hilo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

9FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 878 OF 2023
In the matter of the Estate of the late
SIMBO STEPHEN URASSA
And
In the matter of Application for letters of administration
by
HULDA JOSEPH NGUMA
GENERAL CITATION
(RULE 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 03 day of 10.....2023
Dated at DAR ES SALAAM this 16 day of 08 2023

Senior Resident Magistrate

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 73 OF 2023
In the matter of the estate of the late
SANTIEL YOSIA MKUMBO of IPAGALA
within Dodoma Region.
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION
BY ANA SAMSON MKUMBO
GENERAL CITATION
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23 Day of 08, 2023.
Dated at Dodoma this 9th day of June, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

---

IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 49 OF 2023
In the matter of the estate of the late of the late
FRANK PETRO MUSA
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION
BY OLIVIA PETRO MSAHALA
GENERAL CITATION
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23 Day of August, 2023.
Dated at Dodoma this 2 day of August, 2023.

PETITIONER

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **GEORGE KAHIGI MIHANGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari lenye namba za usajili **T 350 BXR.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/KAG/BUK/80/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0764275751.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**GREGORY ADOLF JOHN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3606/0201/2020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MASUMBWE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020 .Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **GEI/MBO/RB/260554/2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BWANA HOWARD FREDERICK** WA IRINGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T137 CEX** AINA YA SUBARU FORESTER, RANGI NYEKUNDU CHASISI NAMBA **S65008481,** INJINI NAMBA **EJ20692231.** YEYOTE ATAKAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE JALADA NAMBA **PHQ/IRI/IRI/161/2023.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA

WILAYA YA MOROGORO
LILILOPO MOROGORO

MAOMBI NAMBA 79 YA 2023

WELHARD STEVEN MGAYA: ...............MWOMBAJI

DHIDI YA

RICHARD EKIAS GERALD
CHARLES DANIEL KIBWANA
PAULO JOSEPH RHOBI: ......WAJIBU MAOMBI

WITO/KUITWA SHAURINI

**KWA CHARLES DANIEL KIBWANA**
**PAULO JOSEPH RHOBI**

**POPOTE MLIPO** mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 13/09/2023 mbele ya Mwenyekiti E.Mogasa ninyi wenyewe binafsi au mtume wawakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 17 mwezi Agosti 2023.

E. MOGASA
MWENYEKITI

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BWANA SHAMA AMON MGUNDA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T717 BJK AINA YA FUSO MITSUBISHI YENYE RANGI NYEUPE ENGINE NAMBA 6D173691. YEYOTE ATAKAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE JALADA **NAMBA PHQ/IRI/KIL/171/2023.**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**SAKINA J KULEWA,** Anatangaza kupotelewa na vyeti. Cheti cha kidato cha nne chenye index **no.S3466-0118** (Wailes Secondary School) November 2013 ,namba ya cheti Cs130330298. Cheti cha kidato cha sita chenye index no.S0673-0646(Nangwa Secondary School) May 2016,namba ya cheti AC160110368. Cheti za chuo(Muslim University of Morogoro)16 November2019,namba ya cheti BAe 1900094 pamoja na Academic Transcript ya chuo ,pia na cheti cha JKT.Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi **DAR/KIG/RB/271421/2023.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
WILAYA YA MOROGORO
KITUO CHA MJINI
MKOA WA MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi Na......86/2022
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: JOSEPH RAMADHAN MING'EKO WA BIGWA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI
YALIYOLETWA NA GODFREY JOSEPH MING'EKO
TANGAZO
(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 23 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 10 mwezi 08 mwaka 2022

HAKIMU

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**BWANA NUHU HAJI MKEREMY WA** IRINGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ YENYE USAJILI MC 583 CES AINA YA TVS KING RANGI YA KIJANI. YEYOTE ATAKAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE JALADA NAMBA **IRI/IRI/RB/335586/2022.**

---

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**RAFAEL SILVESTER SHAYO** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba: **TAE 147512** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO, mwaka 2019 July. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR /ILA/2306/2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED NASSOR ALI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye usajili namba **T 882 BAP,** CHASSIS NAMBA: **RZJ950027828** na ENGINE NAMBA: **3RZ2108829.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/258228/2023**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA ILALA
(JENGO LA WIZARA YA ARDHI - KIVUKONI)

MAOMBI NAMBA 204 YA MWAKA 2023

PHOENIX OF TANZANIA ASSURANCE COMPANY LIMITED.........................MWOMBAJI

DHIDI YA
DIVINE FORTRESS COMPANY LIMITED.........................MJIBU MAOMBI

KUITWA SHAURINI
DIVINE FORTRESS COMPANY LIMITED ..................POPOTE ULIPO

**PHOENIX OF TANZANIA ASSURANCE COMPANY LIMITED**
Amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala lililopo (Jengo la Wizara ya Ardhi - Kivukoni). Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 13/09/2023. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta utetezi ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala. Endapo hautatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.

Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 17 Mwezi Agosti, Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) – ILALA
DAR ES SALAAM

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA ILALA
(JENGO LA WIZARA YA ARDHI - KIVUKONI)

MAOMBI NAMBA 203 YA MWAKA 2023

PHOENIX OF TANZANIA ASSURANCE COMPANY LIMITED.........................MWOMBAJI

DHIDI YA
DIRMA HOLDINGS TANZANIA LIMITED.........................MJIBU MAOMBI

KUITWA SHAURINI
DIRMA HOLDINGS TANZANIA LIMITED ..................POPOTE ULIPO

**PHOENIX OF TANZANIA ASSURANCE COMPANY LIMITED**
Amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala lililopo (Jengo la Wizara ya Ardhi - Kivukoni). Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 13/09/2023. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta utetezi ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala. Endapo hautatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.

Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 17 Mwezi Agosti, Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) – ILALA
DAR ES SALAAM

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA ILALA
(JENGO LA WIZARA YA ARDHI - KIVUKONI)

MAOMBI NAMBA 202 YA MWAKA 2023

PHOENIX OF TANZANIA ASSURANCE COMPANY LIMITED.........................MWOMBAJI

DHIDI YA
JACOL MEDIA LIMITED.........................MJIBU MAOMBI

KUITWA SHAURINI
JACOL MEDIA LIMITED .........................POPOTE ULIPO

**PHOENIX OF TANZANIA ASSURANCE COMPANY LIMITED**
Amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala lililopo (Jengo la Wizara ya Ardhi - Kivukoni). Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 13/09/2023. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta utetezi ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala. Endapo hautatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.

Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 17 Mwezi Agosti, Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) – ILALA
DAR ES SALAAM

---

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA
LILILOKO DODOMA
MAOMBI NA. 214 YA MWAKA 2023
EDWARD MNYAMAGOLA ..................MDAI
VERSUS
JULIUS NGANGA ..................MDAIWA 1
KABURA ..............................MDAIWA 2
NAOMI OMARI........................MDAIWA 3
ANDREW MATARAGIO.........MDAIWA 4

**KWA:**
**JULIUS NGANGA**
**KABURA**
**NAOMI OMARI**
**ANDREW MATARAGIO**
POPOTE ULIPO.
YAH: KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba wilaya ya Dodoma wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 18.09. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO: kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 21 ya mwezi wa AGOSTI, 2023.


---

THE UNITED PEPUBLIC OF TANZANIA
IN THE DISTRICT COURT OF ARUSHA
AT ARUSHA
CIVIL/APPLICATION/CASE/NO 45 OF 2023
NAHUMU JEREMIAH NANYARO
PLAINTIFF/APPLICATION/D/HOLDER
VERSUS
STRADA INTERNATIONAL B.L.E LTD DEFENDANT/ RESPONDENT/J/DEBTOR

**NOTICE OF HEARING /MENTION**
**TO: STRADA INTERNATIONAL B.L.E LTD**
TAKE NOTICE that the above case has been fixed for mention/hearing in the District Magistrate's Court of Arusha at Arushaon the 15th day of SEPTEMBER 2023 AT 09:00 am O'clock in the forenoon
You may appeal in person or by Advocate or agent duly authorised to appeal on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
TAKE FURTHER NOTICE : That in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence .
GIVEN under my hand and the Seal of the court this 18th day of AUGUST 2023

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**BARAKA BENEDICTOR CHARLES** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S.2870/0050** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHIBULA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MWA/NYA/RB/148402/2021**

---

*OFISI ZA MATANGAZO*
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Tik Tok na Telegram zapigwa 'stop' Somalia

**MOGADISHU,** Somalia

WIZARA ya Mawasiliano na Teknolojia ya Somalia imeagiza mamlaka inayoratibu utoaji wa huduma za intaneti nchini humo kuzima uwezo wa kufikia mitandao ya kijamii ya TikTok, Telegram, na tovuti ya kamari ya 1xBet.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia, Jama Khalif (pichani), alitoa agizo hilo katika taarifa yake iliyotolewa jana, akitaja sababu za kuzuia makampuni hayo kuwa ni usalama na kupambana na ugaidi.

Taarifa hiyo ilisema ukiukaji wa mara kwa mara wa sheria na makundi ya kigaidi yanayotumia mitandao ya kijamii huathiri usalama na utulivu wa jamii.



Wizara hiyo ilisema inafanya kazi kulinda maadili ya watu wa Somalia wakati wa kutumia njia za mawasiliano ya mtandaoni ambazo ilisema zimeathiri mfumo wa maisha na kuongeza kile ilichosema ni tabia mbaya.

"Unaamriwa kuzima mitandao iliyotajwa hapo juu kufikia Alhamisi Agosti 24, mwaka huu, saa kumi na moja jioni, na yoyote ambaye hatafuata agizo hili atakabiliwa na hatua za kisheria zilizo wazi na zinazofaa," alisema Khalif.

Ilielezwa kuwa kundi la wanamgambo wa Al-Shabab mara kwa mara hutumia huduma ya kutuma ujumbe Telegram ili kuchapisha video zake, taarifa kwa vyombo vya habari, na sauti za mahojiano na makamanda wao.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Al-Shabab mara nyingi huchapisha habari kuhusu mashambulizi yake kwenye Telegram na tovuti nyinginezo, ndani ya dakika chache, baada ya kutokea. Kikundi hicho huunda akaunti mpya mara kwa mara pindi tu akaunti zao za Telegram zinapofungwa.

Vile vile, ilibainishwa kuwa TikTok inaaminika kuwa tovuti inayokua kwa kasi zaidi nchini Somalia, na inatumiwa na vijana na hata viongozi wa serikali. **VOA**

## KESI DADA BILIONEA MSUYA

# Shahidi aeleza binti alivyomtambua mtuhumiwa mauaji gwaride la polisi

**Na Grace Gurisha**

MAMALISHE Sophia Shemzigo (46), amedai mahakamani kwamba binti aliyemtambua mtuhumiwa wa mauaji, aliyekuwa mke wa mfanyabiashara marehemu Erasto Msuya, Miriam Mrita, alieleza kuwa huyo ndiye alikwenda nyumbani kwa tajiri wake Kigamboni na akamtishia kwa bastola, akimtaka aondoke.

Sophia alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, wakati akitoa ushahidi wake katika kesi ya mauaji inayomkabili Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wanaotuhumiwa kumuua mdogo wa marahemu Msuya, Aneth Msuya.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Genorosa Montana, Sophia alidai ni mkulima wa mahindi mkoani Songea. Agosti, 2016 alikuwa anaishi na mume wake Kurasini, Dar es Salaam, akijishughulisha na biashara ya mamalishe, eneo la JKT Mgulani. Alidai kuwa Agosti 7, 2016, alikuwa anatoka kudai madeni yake, aliitwa na Askari polisi eneo la Kilwa Road ili ashiriki katika gwaride la utambuzi. Alikubali.

"Akanichukua akanipeleka kituo cha polisi. Nilikuta wanawake wenzangu saba na mimi wa nane, tukapangwa mstari mmoja. Askari akatuambia hapa nimewaita kuna utambuzi, mtuhumiwa wa mauaji anatakiwa atambuliwe.

"Aliletwa mtuhumiwa wa kike (Miriam), akaambiwa achague sehemu yoyote asimame, alichagua nafasi ya tano kutoka kulia na mimi nilikuwa mtu wa wa nne kutoka kushoto. Mwonekano wetu wote ulikuwa wa mfanano, wote weupe, wanene na wafupi wa wastani," alidai.

Shahidi huyo wa 18 aliendelea kudai kuwa, baada ya kupangwa na askari, aliletwa msichana na askari wa kike aliambiwa apite kwenye gwaride mbele na nyuma na amshike mtuhumiwa bega la kushoto.

Alidai kuwa msichana alipomshika begani, alitamka 'huyu ndiye aliyekuja nyumbani kwa tajiri wangu Kigamboni, akanitishia kwa bastola kuwa niondoke'.

"Msimamizi wa gwaride alileta karatasi tukaandika majina yetu, tukatia saini na msimamizi wa gwaride naye akatia saini, tukaruhusiwa kuondoka.

Alianza kutolewa kwanza mtuhumiwa, akafuata binti kutolewa eneo hilo ambapo sijui walikwenda wapi," alidai.

Akijibu maswali ya Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, Sophia alidai kuwa wakati anatoa ushahidi wake akiongozwa na wakili, hakueleza mahakamani kwamba baada ya kumaliza kutia saini karatasi ya gwaride la utambuzi, alitoa namba yake ya simu kwa askari polisi.

**Kibatala: Shahidi wewe unajua Kiingereza hata kidogo?**

**Shahidi:** Hapana

Kibatala: Karatasi uliyojaza ina maneno ya Kiingereza, uliwahi kumweleza jaji na wazee wa baraza kwamba kuna ofisa polisi alikufafanulia ndipo ukajaza?

Shahidi: Sikumwambia Jaji

Kibatala: Hata nikuoneesha hapa kwenye hii karatasi wameandika nine na eighteen kuwa wamesaini?

Shahidi: Mimi sijui, ninajua Kiswahili tu.

**Kibatala: Hapa mahakamani umejitambulisha kwa jina la Sophia Amir Shemzigo, hebu shika hii karatasi utuoneshe ni wapi jaji na wazee wa baraza wataona jina lako?**

**Shahidi:** Hamna Shemzigo ipo Amir.

**Kibatala: Wakati unatoa maelezo yako ulimwambia jaji na wazee wa baraza kuwa mtuhumiwa alikuwa hana pingu?**

**Shahidi:** Sikumwambia

**Kibatala: Ulimwambia jaji kama huyo mama alikuwa ana alama yoyote ya kuweza kumtambua?**

**Shahidi:** Sikumwambia

**Kibatala: Ulimwambia kuwa wewe hauna uhusiano wowote na mwajiriwa wa Jeshi la Polisi?**

**Shahidi:** Sikumwambia

**Kibatala: Ulimwambia kuwa huna chuki wala husda na huyu dada?**

**Shahidi:** Sikumwambia

**Kibatala: Nimekusikia ukitamka maneno ambayo unasema yalitamkwa na huyo binti wa kwenye gwaride.**

**Shahidi:** Eeh

**Kibatala: Ulimsikia akitaja mwezi au tarehe ya siku aliyotishiwa bastola?**

**Shahidi:** Hakutaja tarehe

**Kibatala: Ulimsikia pia binti huyo akisema hata hivyo ninamfahamu huyu mama alikuja kwa mama yangu Mirerani Arusha?**

**Shahidi:** Akacheka

**Kibatala: Mbona unacheka shahidi**

**Shahidi:** Hapana, sikumsikia

Baada ya maswali hayo, Wakili wa Serikali, Paul Kimweri aliomba ahirisho la kesi hiyo hadi leo kwa sababu hawakuwa na shahidi mwingine. Shahidi wa pili waliyekuwa wakimtegemea, alichelewa kufika. Leo watakuwa nao wawili.

**Jaji:** Huyo aliyekuwa amechelewa hawezi kupatikana sasa hivi?

**Kimweri:** Mheshimiwa Jaji, hata tulivyofika hapa hatukuweza kumpata.

**Jaji:** Kwa kuwa hawana shahidi mwingine, ninalazimika kuahirisha kesi hii hadi kesho. Ninawakumbusha upande wa mashitaka kuleta mashahidi na kwa kipindi hicho washitakiwa watakuwa mahabusu," alisema Jaji Kakolaki

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni, jijini Dar es Salaam, amekiri kuhusika na mauaji hayo, katika maelezo yake ya onyo.



Wananchi wakiandamana kuunga mkono serikali ya kijeshi nchini Niger, huku wakisema hawaungi mkono mpango wa nchi za Jumuiya ya Afrika Magharibi (ECOWAS) kuivamia nchi yao. PICHA: REUTERS.

# Waandamana kuunga mkono uongozi wa kijeshi

**NIAMEY,** Niger

MAELFU ya raia wa nchini Niger, wameandamana kuunga mkono uongozi wa jeshi, uliomwondoa madarakani, Rais Mohammed Bazoum (pichani) mwezi uliopita, na kwamba hawaungi mkono mpango wa Jumuiya ya nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) kuvamia kijeshi taifa lao.

Ilielezwa kuwa maandamano hayo yalifanyika jana jijini Niamey, huku waandamanaji wakipeperusha bendera ya nchi yao, wakisikika wakiishutumu Ufaransa na kulaani vikwazo vya kiuchumi vilivyowekewa taifa lao na ECOWAS.

Maandamano hayo yalifanyika siku moja baada ya ujumbe wa ECOWAS ukiongozwa na aliyekuwa kiongozi wa kijeshi nchini Nigeria, Abdulsalami Abubakar kuzuru jijini Niamey kwa ajili ya mazungumzo.

Ujumbe huo ulikutana na uongozi wa kijeshi na Rais Bazoum, huku kiongozi wa ujumbe huo akisema baada ya mazungumzo kuwa bado kuna tumaini la kupata mwafaka kwa njia ya mazungumzo.

Jumamosi iliyopita, kiongozi wa kijeshi Jenerali Abdourahamane Tiani, alionya kuwa jaribio lolote la kuivamia Niger, halitakuwa rahisi na litakabiliwa kwa nguvu.

Aidha, Jenerali Tiani, aliahidi kurejesha madaraka kwa raia baada ya miaka mitatu. **RFI**

# KOCHA AZAM FC AANIKA SABABU YA KICHAPO CAF

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kukubali kichapo cha mabao 2-1 kwenye mechi ya hatua ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bahir Dar Kenema, bechi la ufundi la Azam FC limesema kipigo hicho kimetokana na kucheza na timu ambayo walikuwa hawaifahamu wala hawajawahi kuona video yao yoyote.

Akizungumza na gazeti hili jana kuhusu mchezo huo uliopigwa katika Uwanja wa Abebe Bikila, Addis Ababa nchini Ethiopia. Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, alisema wameshindwa kupata matokeo mazuri kwa kuwa walicheza na timu wasiyofahamu aina ya uchezaji wake.

**"Tumecheza na timu ambayo sijawahi kuona jinsi inavyocheza ndio maana tumeshindwa kufanya vizuri, lakini bado tuna nafasi ya kusonga mbele," alisema Dabo.**

Alisema mchezo ulikuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa na kudai wanajipanga kwa ajili ya mchezo wao wa marudiano utakaochezwa Ijumaa wiki katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Alisema goli moja walilolipata ugenini litawasaidia kufanya vema kwenye mchezo huo kwa kuwa tayari wameshawasoma wapinzani wao.

Alisema hawajakata tamaa kutokana na matokeo waliyoyapata ugenini na badala yake watapambana kuhakikisha wanaingia hatua inayofuata.

Katika mechi hiyo, Azam ilipata bao lake dakika ya 72 likifungwa na straika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Idris Mbombo, aliyeingia akitokea benchi dakika moja kabla ya kucheka na nyavu.

Kwa upande wa magoli mawili ya Bahir Dar Kenema, yalifungwa na Fitsum Gebre dakika ya 20 na 60, ambapo.

Azam sasa inapaswa kushinda angalau bao 1-0 au 2-0 ili kuweza kutinga hatua inayofuata ya raundi ya kwanza ambapo kama ikifuzu itakwenda kucheza dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

**VIPAJI...**



Mchezaji wa timu ya soka Bulls, Talki Seif, akimiliki mpira katikati ya wachezaji wa timu ya Toangoma Youth Soccer, walipokutana kwenye mchezo wa kirafiki uliopigwa Viwanja vya Mikocheni, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mwakinyo kupanda ulingoni Septemba

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Ngumi za Kimataifa (IBA), kipo kwenye mazungumzo na moja ya mabondia kutoka katika mataifa matatu ya Afrika kwa ajili ya kuja nchini kuwania mkanda wao dhidi ya Hassan Mwakinyo katika pambano linalotarajiwa kupigwa Septemba 29, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Mwakinyo ambaye awali alitarajia kupanda ulingoni kuwania mkanda wa Dunia wa WBO kabla ya upepo kubadilika, sasa anatarajia kupanda ulingoni kuwania mkanda wa IBA baada ya pande hizo mbili kufikia makubaliano.

Akizungumza na Nipashe jana, Promota wa pambano hilo kutoka PAF Promotion Company Limited, Ally Mndeme, alisema mpaka sawa mchakato wa kutafuta mpinzani wa Mwakinyo unaendelea vizuri kutoka katika mataifa matatu ya Afrika.

Alisema jukumu la kutafuta mpinzani wa Mwakinyo linashughulikiwa na chama husika cha kimataifa kwa ajili ya kumleta mtu ambaye anaweza kuleta upinzani kwa bondia huyo Mtanzania.

"Tumefikia hatua nzuri katika maandalizi ya awali kwa sababu sehemu kubwa ya hili pambano lipo kwenye kutafuta mpinzani mwenye vigezo vya kucheza na Mwakinyo. Jukumu lipo chini ya IBA wenyewe na mpaka sasa wametuambia wanawasiliana na mabondia kutoka katika mataifa matatu tofauti," alisema Promota huyo.

Alisema hawajaelezwa ni mataifa yapi, lakini wanatarajia kupata mpinzani wake ndani ya Afrika na inaweza kuwa Afrika Kusini, Nigeria au Namibia.

"Katika mataifa hayo matatu mojawapo inawezekana na kama kutakuwa na mabadiliko mengine kuhusu mpinzani lazima watatuambia kwa sababu kwa upande wetu kama waandaji ni lazima tujulishwe," alisema Mndeme.

## Gamondi ashangaa kutoshinda mabao 10

INATOKA UKURASA 24

unacheza kwenye robo tatu ya mpinzani wako halafu hutengenezi nafasi, nina uhakika mechi inayokuja tutaimarisha eneo letu la ufungaji," aliahidi.

Yanga itacheza tena na timu hiyo Jumamosi ijayo, Agosti 26 kwenye uwanja huo huo, ambapo kikanuni Wanajangwani hao watakuwa nyumbani.

Mechi ya juzi ilichezwa nchini baada ya ASAS wenyewe kuamua hivyo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kutokuwa na viwanja vinavyokidhi matakwa ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika, CAF.

Yanga inahitaji ushindi, sare au kufungwa bao lisilozidi moja ili kutinga hatua ya raundi ya kwanza itakayowezesha kucheza na mshindi kati ya Otoho d'Oyo ya Congo Brazaville na El Merrikh ya Sudan ambazo juzi zilitoka sare ya bao 1-1 jijini Brazaville.

Mabao ya Yanga kwenye mechi hiyo yaliwekwa wavuni na Stephane Aziz Ki, na Kennedy Musonda.

## Ajibu afunga bao Ligi Kuu baada ya misimu minne

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Coastal Union, Ibrahim Ajibu, juzi alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya msimu minne kupita.

Ajibu ambaye amesajiliwa na Coastal Union msimu huu, alipachika bao dakika ya 69 kwa mkwaju wa faulo, kwenye mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar, iliyopigwa Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Mara ya mwisho kwa mchezaji huyo kufunga bao kwenye Ligi Kuu ilikuwa ni Januari 15, 2019 akiichezea Yanga ambapo alifunga bao la kwanza dakika ya 13, timu yake ikiichapa Mwadui FC mabao 3-1.

Mabao mengine ya Yanga yalifungwa na Amissi Tambwe na Feisal Salum, huku la kufutia machozi la Mwadui likifungwa na Salum Aiyee.

Msimu huu wa 2018/19, alifunga idadi ya mabao sita akiwa amesajiliwa kutoka Simba 2017 ambapo alirejea tena baadaye kwenye timu yake ya zamani 2019 baada ya msimu wa ligi kumalizika.

Hakuwa na wakati mzuri aliporejea na baadaye akajiunga na Azam FC mwaka 2021hadi 2023 ambapo alikwenda kuichezea Singida Fountain Gate kwa mkopo kipindi cha dirisha dogo msimu wa 2022/23 na baada ya kumalizika msimu huo uliopita, msimu huu amekatua Coastal Union inayonolewa na aliyekuwa Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera.

Hata hivyo, kwenye mechi ya juzi, Mtibwa ilisawazisha bao kupitia kwa Kassim Haruna dakika 10 kabla ya mechi kumalizika.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VERRATTI AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua kiungo wa Paris St-Germain na Italia, Marco Verratti mwenye umri wa miaka 30, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Al-Ahli ya Saudia na mabingwa wa Ujerumani Bayern Munich. ***(L'Equipe, via Mirror)***

### VLACHODIMOS NAYE ATAKIWA

MANCHESTER United pia inachunguza dili la mlinda mlango wa Ugiriki, Odysseas Vlachodimos, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 akitarajiwa kuondoka Benfica. ***(Fabrizio Romano)***

### DOKU AWEKEWA NGUMU

KLABU ya Rennes wamekataa ombi la kwanza kutoka kwa West Ham kumnunua winga wa Ubelgiji, Jeremy Doku mwenye umri wa miaka 21, ambaye pia amevutiwa na Manchester City. ***(Foot Mercato)***

### OLMO AITULIZA RB LEIPZIG

KIUNGO wa kati wa Hispania, Dani Olmo mwenye umri wa miaka 25, amesema "anaridhika" kuwa RB Leipzig baada ya kuhusishwa na uhamisho wa Manchester City kama mbadala wa Kevin de Bruyne aliyejeruhiwa. ***(Bild)***

### TAVARES ATATHIMIWA VILLA

ASTON Villa inatathmini dau la kumnunua beki wa kushoto wa Arsenal na Ureno, Nuno Tavares mwenye umri wa miaka 23, kama mbadala wa mlinzi wa Sevilla mwenye umri wa miaka 31 na Argentina, Marcos Acuna. ***(Fabrizio Romano)***

### FORNALS ATAKIWA SEVILLA

KLABU ya Sevilla inataka kumsajili kiungo wa kati wa West Ham, Pablo Fornals mwenye umri wa miaka 27, ambaye yuko katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake na itaigharimu kati ya pauni milioni 4.3. ***(AS)***

### FOREST YAMTAKA NASCIMENTO

KLABU ya Nottingham Forest iko tayari kulipa pauni milioni 15 kwa mshambuliaji wa Botafogo, Matheus Nascimento, lakini Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 19, anataka uhamisho wake ufanyike Januari ili kusaidia timu yake kushinda taji la Serie A la Brazil. ***(Sun)***

### ADAMS AKARIBIA EVERTON

KLABU ya Everton inakaribia kumsajili mshambuliaji wa Southampton, Che Adams mwenye umri wa miaka 27 kutoka Scotland. ***(Telegraph)***


### DEST HUYOOO PSV

BEKI wa pembeni wa Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 22, atahama kwa mkopo kutoka Barcelona kwenda PSV Eindhoven baada ya mabingwa hao wa La Liga kukubali kulipa asilimia 50 ya mshahara wake. ***(Fabrizio Romano)***

### SANE AFUATILIWA BARCA

BARCELONA wanamfuatilia winga wa Bayern Munich na Ujerumani, Leroy Sane na wanaweza kutuma ofa ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 msimu ujao. ***(Bild, via Goal)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# CANCELO SASA AKARIBIA KUJIUNGA NA BARCELONA

**BARCELONA,** Hispania

●●● Ofa ya kucheza kikosi cha kwanza chini ya Xavi huko Barca imemvutia hivyo...

BARCELONA ina uhakika wa kukamilisha uhamisho wao wa kumnunua Joao Cancelo wiki hii, vyanzo vimeiambia 90min.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, hana nafasi kule kwenye Uwanja wa Etihad chini ya Kocha Pep Guardiola.**

Alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo kule Bayern Munich, ambao walikataa kumsajili kwa uhamisho wa kudumu.

Baada ya mazungumzo mazuri mwishoni mwa juma, Barca sasa wanakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili Cancelo kwa mkopo kwa msimu huu.

Vyanzo vya habari vimethibitisha kwamba Barcelona itagharamia sehemu kubwa ya mshahara wa Cancelo katika msimu huu na pia wamekubali chaguo lenye thamani ya pauni milioni 30 ili kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu msimu ujao.

Cancelo alipata ofa kutoka Saudi Arabia na pia kulikuwa na nia kutoka Ulaya, ikiwa ni pamoja na Arsenal, lakini ofa ya kucheza katika kikosi cha kwanza chini ya Xavi huko Barca lilikuwa chaguo la kwanza la mchezaji huyo.

Nyota huyo huenda akapata nafasi ya kuungana na mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Ureno, Joao Felix, huku mazungumzo yakiendelea kuhusu mkataba wa mkopo na Atletico Madrid.

Makamu wa rais wa Barcelona, Rafa Yuste, hivi karibuni alikiri kwa Movistar kuwa klabu hiyo ilikuwa na matumaini ya kuwapata Cancelo na Felix.

"Ni jambo la kujivunia kwa klabu kwamba Joao Felix anazungumza kwa njia hiyo kuhusu Barcelona, lakini kuna operesheni mbili ambazo Xavi na Deco wanapaswa kushughulikia," alisema Yuste.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 681,

MECHI KALI
SINGIDA BS FC
VERSUS
TANZANIA PRISONS
1 | 1.74
X | 3.23
2 | 4.87

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BELLINGHAM: KWA SASA MIMI NI BORA MARA 10

**MADRID,** Hispania

JUDE Bellingham amesema amekuwa "bora mara 10" kuliko alivyokuwa msimu uliopita katika Klabu ya Borussia Dortmund baada ya kuendelea na maisha yake mazuri akiwa Real Madrid kwa mabao mawili na kusaidia katika ushindi wa 3-1 kwenye LaLiga dhidi ya Almeria, Jumamosi.

Bellingham amezoea maisha ya Madrid haraka tangu uhamisho wake wa euro milioni 103 kutoka klabu hiyo ya Bundesliga, akifunga bao katika ushindi wao wa 2-0 dhidi ya Athletic Club wikendi iliyopita kabla ya mabao mawili Jumamosi kwenye Uwanja wa Power Horse.

"Nadhani mimi ni mchezaji bora mara 10 kuliko msimu uliopita," Bellingham aliiambia Real Madrid TV.

"Ninajifunza kutoka kwa wachezaji hawa. Kiwango cha hapa ni cha juu sana."

Sergio Arribas aliiweka mbele Almeria mapema kabla ya Bellingham kusawazisha dakika ya 19 na kisha kuiweka Madrid mbele kwa bao la kichwa, kabla ya Vinicius Junior kufunga la tatu.

"Niliona Real Madrid ikirejea mara nyingi kwenye TV nilipokuwa mtoto," alisema Bellingham.

"Nakumbuka nilifikiri hawataweza na mwisho walifanya hivyo, sasa nipo na naona, sikuwahi kufikiria kuwa tutapoteza, niliangalia nyuso za wachezaji na hakukuwa na hofu."

Baada ya kufunga bao lake la kwanza msimu huu, Vinicius alisema anatumaini ushirikiano wake na Bellingham unaweza kufikia lile aliloshiriki na mchezaji mwenzake wa zamani, Karim Benzema.



## Guardiola asifu kiwango cha Fode

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola alisifu kiwango cha Phil Foden baada ya Manchester City kuendeleza mwanzo wao mzuri wa ushindi wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Newcastle United.

Julian Alvarez alifunga bao pekee katika mchezo mkali uliochezwa kwenye Uwanja wa Etihad Jumamosi, lakini Foden ndiye aliyemwagiwa sifa nyingi zaidi.

Kiungo huyo wa kati wa England, Foden alicheza vizuri na Alvarez katika dakika ya 31 na kusababisha kupatikana kwa bao hilo na alionekana kuwa na uwezo zaidi wa kuziba pengo la Kevin De Bruyne ambaye ni majeruhi.

"Nimesema mara nyingi, Phil anaweza kucheza katika nafasi zote za mbele," alisema Guardiola.

"Ana uwezo wa ajabu. Jinsi anavyogeuka na kushambulia ni mojawapo ya bora zaidi ambayo nimeona.

"Kila udhibiti, anajua hasa lengo ni nini. Hahitaji miguso miwili au mitatu ili
pata nafasi sahihi ya k
ambulia lango. Kwa mg
mmoja tu anashambulia

"Makocha hurekeb
ujuzi kwa wachezaji
lionao, au matatizo tu
nayo hivi sasa. Phil, an
jinsi alivyo katika na
hiyo, jinsi alivyo mzuri k
mshambuliaji au winga
kushoto au winga.

"Bado hatuko kwe
ubora wetu, bado tuna
wa kupiga hatua, lakini
ni kawaida kabisa ka
kipindi cha aina hii.

# 245,750

## JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/08/23 | 22:00 | Molde vs Galatasaray | 2.75 | 3.40 | 2.39 |
| 02. 23/08/23 | 22:00 | Maccabi Haifa vs BSC Young Boys | 2.30 | 3.41 | 2.76 |
| 03. 23/08/23 | 23:00 | Vargas Torres vs Imbabura Sporting Club | 2.66 | 3.01 | 2.55 |
| 04. 24/08/23 | 02:00 | FC Cincinnati vs Inter Miami CF | 3.06 | 3.84 | 2.03 |
| 05. 24/08/23 | 03:00 | Tulsa Roughnecks vs Birmingham Legion FC | 2.41 | 3.41 | 2.55 |
| 06. 24/08/23 | 06:00 | San Luis vs Club Leon | 2.38 | 3.32 | 2.75 |
| 07. 24/08/23 | 18:00 | FC Struga Trim Lum vs Breidablik | 2.43 | 3.30 | 2.75 |
| 08. 24/08/23 | 20:00 | Sepsi Osk vs Bodo Glimt | 3.25 | 3.30 | 2.13 |
| 09. 24/08/23 | 20:00 | Dynamo Kiev vs Besiktas | 2.85 | 3.35 | 2.34 |
| 10. 24/08/23 | 21:00 | Olimpija Ljubljana vs Karabakh | 2.65 | 3.20 | 2.55 |
| 11. 24/08/23 | 21:30 | Osasuna vs Brugge | 2.17 | 3.36 | 3.11 |
| 12. 24/08/23 | 21:30 | Slovan Bratislava vs Aris Limassol | 2.20 | 3.20 | 3.20 |
| 13. 24/08/23 | 21:45 | Hearts vs PAOK | 2.55 | 3.30 | 2.60 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 22/02/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1280 | Hyundai Steel W vs Daejeon Sportstoto W | 1.24 | 5.50 | 8.76 |
| 13:00 | 2004 | Portimonense U23 vs Benfica U23 | 2.41 | 3.32 | 2.60 |
| 13:00 | 2823 | Changnyeong W vs Busan Sangmu W | 2.36 | 3.15 | 2.65 |
| 13:00 | 2856 | Suwon Fmc W vs Seoul City W | 1.50 | 3.96 | 5.48 |
| 13:00 | 4374 | Hwacheon Kspo W vs Gyeongju WFC W | 2.37 | 3.11 | 2.80 |
| 14:00 | 5695 | Cardiff City U21 vs Sheffield Wednesday U23 | 1.51 | 4.77 | 4.36 |
| 14:30 | 2706 | Shanghai SIPG vs Bangkok Glass | 1.09 | 7.49 | 19.24 |
| 14:30 | 5307 | Hangzhou NG vs Port FC | 1.51 | 4.01 | 5.28 |
| 15:00 | 1292 | Bristol City U23 vs Sheffield United U23 | 3.51 | 3.91 | 1.79 |
| 15:30 | 3073 | Ipswich U23 vs Birmingham U21 | 1.84 | 4.08 | 3.22 |
| 16:00 | 2106 | Singida BS FC vs Tanzania Prisons | 1.74 | 3.23 | 4.87 |
| 16:00 | 2635 | Penang vs Kedah | 3.83 | 3.83 | 1.70 |
| 17:30 | 1650 | Estoril Praia U23 vs CD Mafra U23 | 1.48 | 4.20 | 5.32 |
| 18:00 | 1739 | Estrela Amadora U23 vs SC Farense U23 | 2.05 | 3.17 | 3.37 |
| 18:00 | 5139 | SP. Braga U23 vs Rio Ave U23 | 1.66 | 3.72 | 4.38 |
| 18:00 | 5905 | Leixoes SC U23 vs FC Vizela U23 | 2.44 | 3.36 | 2.54 |
| 18:30 | 3506 | AL Wakrah vs Navbahor Namangan | 2.29 | 3.20 | 2.85 |
| 19:00 | 3182 | Teraktor Sazi vs Al Sharjah SC | 1.89 | 3.21 | 3.87 |
| 19:00 | 5999 | SK Hranice vs Unicov | 6.33 | 4.39 | 1.40 |
| 19:05 | 5561 | AL Qaisoma vs Al Jabalain | 2.20 | 2.93 | 3.18 |
| 19:30 | 2779 | SV Horn vs FC Liefering | 2.75 | 3.62 | 2.17 |
| 20:00 | 1404 | Preussen Munster vs Ingolstadt | 2.39 | 3.36 | 2.74 |
| 20:00 | 1659 | FC Fredericia vs Horsens | 2.57 | 3.37 | 2.36 |
| 20:00 | 2050 | SSV Ulm vs Arminia Bielefeld | 3.21 | 3.42 | 2.10 |
| 20:00 | 2501 | Hallescher vs Duisburg | 2.43 | 3.37 | 2.70 |
| 20:00 | 2521 | Naestved BK vs B 93 Copenhagen | 2.21 | 3.43 | 2.73 |
| 20:00 | 3023 | 1860 Munich vs VfB Lubeck | 1.68 | 3.69 | 4.67 |
| 20:00 | 3180 | Dynamo Dresden vs Waldhof Mannheim | 1.68 | 3.72 | 4.66 |
| 20:20 | 4315 | Al Nasr Riyadh vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 1.14 | 6.52 | 14.26 |
| 21:00 | 3920 | Walsall vs Brighton U23 | 2.34 | 3.67 | 2.50 |
| 21:00 | 4882 | Swindon Town vs Arsenal U21 | 2.26 | 3.77 | 2.55 |
| 21:30 | 2680 | Deportivo Paraguayo vs Central Ballester | 2.50 | 2.60 | 2.95 |
| 21:30 | 3071 | Stockport vs Manchester United U21 | 1.82 | 3.77 | 3.52 |
| 21:45 | 1168 | Crusaders Belfast vs Carrick Rangers | 1.33 | 4.85 | 6.47 |
| 21:45 | 2270 | Whitby Town vs Worksop Town | 2.28 | 3.46 | 2.69 |
| 21:45 | 2323 | Matlock Town vs Atherton Collieries | 1.71 | 3.55 | 4.26 |
| 21:45 | 2480 | Hyde United FC vs Marine FC | 2.12 | 3.31 | 3.06 |
| 21:45 | 2894 | Utd of Manchester vs Ilkeston Town FC | 2.43 | 3.62 | 2.42 |
| 21:45 | 3379 | Lancaster City vs Macclesfield FC | 4.79 | 3.87 | 1.58 |
| 21:45 | 4116 | Portsmouth vs Fulham U23 | 1.72 | 3.93 | 3.77 |
| 21:45 | 4279 | Linfield Belfast vs Cliftonville Belfast | 1.70 | 3.63 | 4.03 |
| 21:45 | 4350 | Marske United FC vs Bamber Bridge | 2.75 | 3.46 | 2.24 |
| 21:45 | 4861 | Basford United vs Stafford Rangers | 2.36 | 3.36 | 2.64 |
| 21:45 | 5256 | Gainsborough vs Guiseley | 2.01 | 3.51 | 3.16 |
| 21:45 | 5460 | Warrington Rylands 1906 FC vs Ashton Utd | 1.84 | 3.67 | 3.51 |
| 21:45 | 5602 | Falkirk FC vs Stirling | 1.59 | 3.77 | 4.99 |
| 22:00 | 1360 | Rangers vs PSV Eindhoven | 2.60 | 3.50 | 2.46 |
| 22:00 | 3229 | Royal Antwerp vs AEK Athens | 2.14 | 3.45 | 3.10 |
| 22:00 | 3940 | Rakow Czestochowa vs Copenhagen | 2.35 | 3.30 | 2.85 |
| 23:00 | 4982 | Comerciantes FC vs Deportivo Llacuabamba | 1.87 | 3.33 | 3.64 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SPORTPESA, TIGO PESA SASA ZAJA NA 'MAOKOTO DEILEE'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI namba moja ya Michezo ya Kubashiri nchini, SportPesa, kwa kushirikiana na mtandao wa tiGO kupitia huduma ya tiGO Pesa zimezindua kampeni inayoitwa 'Maokoto Deilee', lengo likiwa ni kutoa fursa ya kujishindia zawadi mbalimbali kwa wateja wao.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya, akizungumza jijini Dar es Salaam jana katika hafla fupi ya uzinduzi wa promosheni hiyo, alisema promosheni hiyo inampa nafasi kila mtumiaji wa mtandao wa tiGO kuweza kujishindia zawadi hata kama atakosa matokeo ya bashiri zake.

"Mteja akishaweka pesa kwenye akaunti yake ya SportPesa kupitia tiGO Pesa na kisha kuweka bashiri yake, anapata fursa moja kwa moja ya kuingia kwenye droo ya wiki. Wateja wetu wana fursa ya kujishindia zawadi za kila siku Sh. 20,000, zawadi za wiki shilingi milioni moja na zawadi kubwa ya Sh. milioni 15. Pia kila wiki washindi wawili wataweza kujinyakulia simu janja.

"'Maokoto Deilee' inawapa nafasi wateja wa SportPesa na tiGO Pesa kujishindia zawadi za pesa kila siku, wiki pamoja na simu janja huku zawadi kubwa kabisa ikiwa ni kiasi cha shilingi milioni 15 ambacho kitatolewa mwisho wa promosheni.

Kuhusu ushirikiano huo, Meneja Biashara wa tiGO Pesa, Kenneth Ndulute, alisisitiza kampeni hiyo ni fursa kwa wateja wao kujishindia zawadi mbalimbali huku wakibashiri mechi wazipendazo kupitia mtandao wa tiGO.

Ndulute aliwahimiza wateja kuchangamkia fursa hiyo kwa kushiriki katika kampeni ya 'Maokoto Deilee' ili waweze kujishindia zawadi hizo.

Aidha, wateja wa tiGO Pesa ambao hawana akaunti ya SportPesa, wanaweza kufungua akaunti kwa kutembelea tovuti ya sportpesa.co.tz au kupakua App ya SportPesa au kupiga *150*87#.

Baada ya kufungua akaunti, mteja anaweza akaweka fedha kwenye akaunti yake ya SportPesa kwa kutumia tiGO Pesa.




Kutoka kushoto ni Mkaguzi wa Bodi ya Michezo ya Kubashiri, Rasul Masoud, Meneja Biashara wa tiGO Pesa, Kenneth Ndulute, Mkuu wa Idara ya Uhusiano na Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya, Mkuu wa Idara ya Masoko SportPesa na Meneja Biashara tiGO Pesa, Fabian Felician, wakionesha zawadi kubwa atakayopata mshindi kwenye 'Maokoto Deilee', wakati wa uzinduzi wa promosheni hiyo Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Phiri atangaza vita, Robertinho naye afunguka

INATOKA UKURASA 24

niweze kukata kiu ya mashabiki wetu," alisema Phiri.

Aliongeza kuwa hawezi kuahidi atafunga mabao mangapi kwa sababu matarajio yake na wenzake ni kuhakikisha msimu huu mashabiki wao wanapata furaha kwa kupambana kusaka pointi tatu muhimu kwa kila mechi.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliviera, alisema anataka kuona mpira mzuri na anaona mwelekeo wa timu yake kutandaza kabumbu ambalo anataka kuliona ndani ya kikosi cha Wekundu wa Msimbazi hao.

Robertinho alisema wachezaji wapya waliosajiliwa msimu huu wanapewa nafasi na wanaonesha uwezo mkubwa ambapo wanaingia taratibu kikosini.

Alisema nyota wapya na wale waliokuwapo awali wameweza kutengeneza muunganiko mzuri na kupata mwelekeo wa timu yake kucheza soka ambalo analihitaji la 'Samba Loketo'.

"Nahitaji kuona mpira mzuri, mpira sio ugomvi ni kipaji na sanaa, napenda kushambulia zaidi na kucheza mpira mzuri, matarajio yangu muda mfupi naweza kupata mwelekeo wa kile ninachokitaka katika kikosi changu.

"Nimefurahishwa na kiwango kilichooneshwa na wachezaji wangu hasa wale tuliowasajili msimu huu wanaonesha kiwango bora na kadiri wanavyopata muda wa kucheza wanazidi kuimarika," alisema Robertinho na aliongeza:

"Kadri siku zinavyozidi kwenda wachezaji wanazidi kuzoeana, mimi nimetoka Brazil, nimecheza soka na sasa ni mwalimu mara zote naamini kwenye soka la kushambulia pamoja na kumiliki mchezo na hicho ndio nataka wachezaji wangu wakifanye."

Aidha, aliwapongeza wapinzani wao, Dodoma jiji FC kwa kuonesha soka zuri na kuweza kuzuia mipango yao katika dakika 44 za kipindi cha kwanza kabla ya kuruhusu bao la kwanza.

# Michezo

Jumanne Agosti 22, 2023

Nipashe





Guardiola asifu kiwango cha Foden UKURASA 22

# Gamondi ashangaa kutoshinda mabao 10

### ●●● Alia kufanya mazoezi uwanja nyasi halisi huku mechi CAF wakicheza katika nyasi bandia, aahidi...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema pamoja na kushindi wa mabao 2-0 dhidi ya ASAS Ali Sabieh ya Djibouti juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, uliopo Chamazi, Dar es Salaam, hajafurahishwa na idadi ya mabao akisema kama safu ya ushambuliaji ingetulia, wangeshinda 10-0.

**Akizungumza baada ya kumalizika mechi hiyo ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kocha huyo raia wa Argentina alisema hakufurahishwa pia na jinsi walivyocheza kipindi cha kwanza, lakini timu iliamka kipindi cha pili ingawa changamoto ilikuwa ni kukwamisha mpira ndani ya wavu.**

"Mabao hayakutosha, mabao mawili kwenye mchezo wa mpira siyo tofauti kubwa hasa mechi hizi za mtoano na zenye marudiano, mchezo bado upo wazi ulikuwa ni mchezo wa ugenini sasa tunatakiwa kucheza dakika 90 za nyumbani ili kumaliza kazi, niseme tu kwenye mechi hii tumepoteza nafasi nyingi sana, kama tungekuwa vizuri kwenye umaliziaji leo tungeshinda hata mabao 10-0, inawezekana kushindwa kufunga idadi hiyo ya mabao, lakini angalau ingekuwa karibu na hapo," alisema kocha huyo.



Hata hivyo, aliitaja changamoto nyingine kwamba walikuwa wakifanya mazoezi kwenye uwanja wenye nyasi halisi, lakini kwenye mechi wamecheza katika nyasi bandia, hivyo kupunguza baadhi ya vitu vya kiufundi kwa wachezaji wake.

"Siku furahia mchezo ambao timu yangu imecheza kipindi cha kwanza na nadhani tulifanya mazoezi kwenye kiwanja cha nyasi, lakini mechi tumekuja kucheza katika uwanja wa nyasi bandia," alisema.

Aliahidi kwa siku zilizobaki kubadilisha baadhi ya mambo ikiwamo kuimarisha eneo la mwisho kwenye umaliziaji ili kuweza kupata idadi kubwa ya mabao.

"Nakwenda kulifanyia kazi ili kubadilisha baadhi ya mambo, uzuri ni kwamba tunatengeneza nafasi, kibaya ni kwamba

INAENDELEA UKURASA 20




AJIBU

## Ajibu afunga Ligi Kuu baada ya misimu minne

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Coastal Union, Ibrahim Ajibu, juzi alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara

INAENDELEA UKURASA 20

## Phiri atangaza vita, Robertinho naye afunguka

**Na Saada Akida**

BAADA ya juzi kufunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu wa 2023/24, Mshambuliaji wa Simba, Mosses Phiri, ametangaza hali ya hatari kwa mabeki wa timu pinzani kwa kueleza amerejea upya akiwa na lengo la kucheka na nyavu zaidi kila atakapopata nafasi ndani ya kikosi cha timu hiyo.

Katika mchezo wa juzi dhidi ya Dodoma Jiji FC uliopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na Simba kushinda mabao 2-0, Phiri aliingia dakika ya 53 na kufunga bao lake la kwanza kwenye mechi yake ya pili ya ligi hiyo akiingia uwanjani kuchukua nafasi ya Jean Baleke, ambaye aliitanguliza mbele timu na kuifanya kuongoza 1-0 kipindi cha kwanza.

Akizungumza na Nipashe juzi baada ya kukamilika dakika 90 za mchezo huo, Phiri alisema amefurahi sana kufunga bao lake la kwanza kwenye mechi hiyo ya ligi ikiwa ni kipindi kirefu tangu aumie msimu uliopita.

Alisema anatumai ataendelea kufunga zaidi kila anapopata nafasi ya kucheza na kufanya kile alichokifanya msimu uliopita kwa kufunga jumla ya mabao 10 kabla ya kupata majeraha.

"Nafurahi kucheza mechi na kufunga bao, ninaimani kwa kushirikiana na wenzangu nitawapa furaha mashabiki wa Simba na kuhakikisha tunapambana kufikia malengo wanayoyatarajia ikiwamo kushinda kila mechi.

"Matarajio yangu ni kufunga zaidi kila ninapopata nafasi ya kucheza, msimu uliopita nilifunga mabao 10 na sikuweza kuendelea kwa sababu ya majeraha, ninaimani na ninamuomba Mungu kunijalia afya njema ili

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >